

**Romy** Jones kuja kivingine

UKURASA 20



**Chelsea** yajipanga kwa Haaland

UKURASA 21

## MAISHA

JUNI 27, 2021 Nipashe — Baba, Mama na Mwana — *Jumapili*



Ukurasa 14

**Vyakula vya kupunguza unene**



Ukurasa 15

**MAISHA NI NYUMBA**
Hivi ndivyo unapaswa kuandaa chumba cha mtoto







UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Juni 27, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580624

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


## SIKU 100 IKULU

# Mama 'aupiga mwingi'




## Rais Samia aliamsha Bandari ya Bagamoyo

UKURASA 2



### RIPOTI MPYA

# Ajali zinaathiri nguvu za kiume

UKURASA 3





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play — Download on the App Store


**MICHEZO** SIMBA YAIFUATA YANGA FAINALI UK.24 — MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara Tanzania (TNBC), Rais Samia Suluhu Hassan, akifungua mkutano wa 12 wa Baraza hilo, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Samia aliamsha Bandari ya Bagamoyo

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema serikali imeanza mazungumzo ya kutekeleza mradi wa Bandari ya Bagamoyo na ule wa Mchuchuma na Liganga.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara ambalo Rais ni mwenyekiti wake.

Rais Samia alisema wanakwenda kuanza mazungumzo na taasisi iliyokuja kwa ajili ya mradi wa Bagamoyo ili waufungue na kwenda nao kwa manufaa ya taifa.

Kuhusu Liganga na Mchuchuma, Rais alisema ameshatoa maelekezo kwa sekta husika ambazo zinaendelea na mazungumzo na wawekezaji kuona tatizo lilipo.

"Waone tatizo ni nini hasa na serikali inaweza kujitoa mpaka wapi na mwekezaji ajitoe mpaka wapi, lakini ule mradi uende kufanya kazi na taarifa zilizopo duniani sasa chuma kimepanda bei, hivyo ni wakati mzuri wa kuharakisha na kufanya huo mradi," alisema.

Akizungumzia baraza hilo, Rais Samia alisema ufanisi wake utatokana na mabaraza ya mikoa na wilaya na kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kushirikiana na sekretarieti ya taifa kuhakikisha mabaraza katika ngazi hiyo yanafanya kazi.

"Kupitia baraza hili na kupitia taasisi binafsi, kumeundwa majukwaa ya wanawake peke yao. Kwa hiyo, wakuu wa mikoa na wilaya wakiendelea kuyasimamia mabaraza haya yatafanya kazi vizuri, nami nimejitolea kuwa mlezi wa mabaraza haya ya wanawake," alisema.

Rais Samia alisema alikutana na sekretarieti ya sekta binafsi na alipokea mambo mengi na aliagiza yafanyiwe kazi na yameingizwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22.

Pia alisema wamefanya kazi kubwa ya kuikuza Benki ya Maendeleo ya Kilimo na ya Uwekezaji kwa kuziongeza mitaji na wanatarajia kuiongeza zaidi ili kuwawezesha wafanyabiashara kutoka hatua moja kwenda nyingine kujenga uchumi wa nchi.

Alisema jambo lingine ambalo serikali inakwenda kuliwekea mkakati mkubwa ni sekta ya utalii ambayo iliathiriwa na janga la corona.

Rais pia aliahidi kufanyia kazi uanzishwaji wa sera ya maendeleo ya sekta binafsi.

Pia aliahidi serikali kuiangalia Sheria ya Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) ikiwa ni pamoja na kujua kwa nini ilitungwa.

"Suala la ukaguzi wa magari, yalikuwa yanakaguliwa huko na baadaye yanafanyiwa ukaguzi wa pili hapa (Tanzania), ni wafanyabiashara nyie mlilipigia kelele miaka ile kwa nini yanafanyiwa ukaguzi wa awali kule serikali ikawasikiliza, tunafanya hapa sasa ni kelele nyingine.

"Tutakaa tuangalie wapi panapotuchoma, tupunguze makali ili twende vizuri," alisema.

Rais Samia alisema kwa sasa wapo katika wimbi la nne la mapinduzi ya viwanda ambalo limeangukia Afrika.

"Lazima tulitumie vizuri wimbi hili la mapinduzi ya nne ya viwanda kwa sababu limekuja na maendeleo ya teknolojia, ni vyema tukajipanga kwa uwezo wetu tukalitumia kwenye ICT (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano), lengo ni mazingira ya biashara yawe mazuri tukuze uchumi," alisema.

# Hoja 18 za sekta binafsi kwa Rais Samia

**Na Romana Mallya**

SEKTA Binafsi imeainisha mambo 18 ambayo inayatarajia kwa serikali katika utekelezaji na maboresho, huku ikilalamikia uamuzi wa Shirika la Viwango (TBS) kukagua magari yanayoingizwa nchini, kwamba unasababisha magari mabovu kuingizwa kwa wingi nchini.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi (TPSF), Angelina Ngalula, aliwasilisha matarajio yao hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam mbele ya Rais Samia Suluhu Hassan, wakati wa mkutano wa 12 wa Baraza la Taifa la Biashara.

Akizungumzia taasisi za udhibiti, Ngalula alisema sekta binafsi inaomba zijikite kwenye kutoa elimu na maarifa ya kuongeza ubora wa bidhaa za Tanzania ili zishindane kwenye soko la kanda na kimataifa badala ya kufanya biashara.

Kiongozi huyo alisema Shirika la Uwakala wa Meli (TASAC) nalo limekuwa ni kero kwa kuwa badala ya kushughulika na kuboresha usafiri wa majini, limeingia kwenye biashara na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara.

Jambo la pili alilitaja kuwa ni uharakishwaji wa Blue Print na la tatu ni uharakishwaji wa sera na sheria ya uwezeshaji wa Tanzania.

Jambo la nne na la tano ni kuwapo sera tulivu zinazotabirika ili kukuza na uwekezaji na miradi inayotekelezwa kwa ushirikiano wa sekta binafsi na sekta ya umma (PPP) iainishwe ili sekta binafsi ziungane na wawekezaji wa nje kushiriki kwa ubia na serikali, mtawalia. Ngalula alitaja jambo la sita ni uendelezaji na uwekezaji kwenye miundombinu wezeshi ya barabara na reli ya kisasa.

Jambo la saba waliloomba serikalini ni kutoa kipaumbele kwa vijana kupatiwa ujuzi na stadi za kazi.

"Jambo la nane, mifuko ya udhamini kwa ajili ya mitaji kwa ajili ya biashara ndogo na za kati, tisa ni urasilimishaji wa biashara za wajasiriamali wadogo ili kuwatengenezea mazingira bora na kupanua wigo la walipa kodi, jambo la 10 ni kuongeza mtaji katika benki ya kilimo kwa ajili ya miradi mikubwa," alisema.

Alitaja hoja yao ya 11 ni serikali kuwekeza katika utafiti kwa wizara kuwa na vitengo ambavyo vitakuwa na jukumu la kuibua fursa za kiuchumi.

Mengine ni kuiamini sekta binafsi katika eneo la ujenzi, kutumia takwimu na teknolojia ili kufanya makadirio ya kodi hasa eneo la forodha, serikali kutilia mkazo utalii wa fukwe na wizara na sekta binafsi kushirikiana kutengeneza mkakati wa pamoja ili kuongeza watalii wa ndani na nje kwenda Mikumi na Ruaha kupitia reli ya kisasa.

Lingine ni ushirikiano wa kiuchumi na wa kibiashara kikanda kwa kuangalia ufanisi wa sheria.

Alitaja hoja nyingine ni malipo ya malimbikizo ya madeni ya wafanyabiashara na marejesho ya Kodi la Ongezeko la Thamani (VAT).

"Suala la 18 ni Bandari ya Bagamoyo, inahitajika sana, tulileta hoja za sekta binafsi kutokana na maendeleo yanayoendelea kwenye kanda na Bandari ya Dar es Salaam kuwa ni ndogo na haiwezi kuongezwa.

# Wabaini tatizo mabasi nchini

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA-CCC) limeishauri serikali katika kukabiliana na ajali za barabarani, ifanye utafiti wa mabasi yaliyojengwa kwa kutumia chesesi ya malori ili iliyafute kwa madai si salama.

Mwenyekiti wa LATRA-CCC, Dk. George Makuke, aliyasema hayo mkoani Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa Jukwaa la Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) ambao ni wadau wa usafiri.

Alisema baadhi ya mabasi yanayotoa huduma za usafirishaji, yamejengwa kwa kutumia chesesi za malori ambayo siyo salama.

"Suala hili limetokea kwa sababu utafiti wa kina haujafanyika, kilichotokea ni kwamba ushuru wa kuagiza lori ni kidogo kulinganishwa na kuagiza basi.

"Wenye mabasi wamechukua mwanya huo kwa kwa kuziangalia chesesi zinafanana lakini muundo ni tofauti," alisema.

Kuhusu ubora wa basi, Makuke alisema abiria anaweza kubaini anapoingia ndani yake ama kwa namna lilivyo au bei ya nauli kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

"Unakuta usafiri kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, abiria unaambiwa lipa hata Sh. 30,000 badala ya Sh. 50,000, unapaswa ujiulize 'tatizo ni nini?' Maana mafuta yanayotumika ni hayo hayo ya dizeli, vipuri ni bei ni ile ile," alisema.

Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya LATRA-CCC, Henry Bantu, alisema sheria inayoleta matatizo ni ya zamani ambapo walisisitiza maendeleo ya vijijini yanayohitaji malori.

"Mabasi mengi mnayoyaona sasa chesesi zake ni za lori lakini yale mabasi yaliyoumbwa kama mabasi yana vikorombwezo vingi vya usalama," alisema.

Kaimu Katibu Mtendaji wa LATRA-CCC, Leo Ngowi, alisema kaulimbiu yao ni 'LATRA-CCC Sauti ya Jamii' kwa maana kwamba wapo tayari kupaza sauti kwa ajili ya watumiaji kwa yale mambo ambayo hawafurahishwi nayo.

Alisema jukwaa hilo ni mwendelezo wa mengine ambayo watayazindua katika vyuo kikiwamo Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kwa lengo la kupata wadau wengi wasomi katika sekta ya usafiri ili kufanya utafiti utakaosaidia kuleta mabadiliko chanya katika uchumi.

Mwenyekiti na Mwasisi wa Jukwaa hilo, Faizaki Musa, alishukuru LATRA-CCC kwa kuona umuhimu kwa wanafunzi ambao ni waathirika wa ajali za barabarani, kutoa maoni na ushauri kwa serikali ili kubadilisha mfumo, sera na kanuni mbalimbali katika utoaji huduma za usafiri.

## HABARI KITAIFA




Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akihutubia katika hafla ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kupiga Vita Matumizi na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya Duniani, jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Ajali zapunguza nguvu za kiume

**Na Christina Mwakangale**

IMEBAINIKA kuwa baada ya matibabu ya kibingwa ambayo hufanyiwa madereva waliopata ajali, wanaopona hukumbwa na adha ya kupungukiwa au kukosa kabisa nguvu za kiume.

“Chumba cha upasuaji MOI mara nyingi huwa kiko ‘busy’, iwe dharua au upasuaji wa kawaida.

“Mrejesho wa wale tunaowatibu kutokana na matukio ya ajali, wanasema wanashindwa kushiriki tendo la ndoa.

“Mtu anakuja anakwambia sasa hivi siwezi kabisa, dokta nimepona, ninatembea lakini siwezi...”

Ni kauli ya Bingwa wa Magonjwa ya Ajali na Mifupa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Kenedy Nchimbi.

Alitoa kauli hiyo wakati wa mafunzo ya siku tatu kuhusu usalama barabarani kwa madereva wa safari ndefu za ndani na nje ya nchi jirani iliyofanyika jijini Dar es Salaam wiki hii.

Takwimu zilizotolewa na Kitengo cha Uhusiano cha MOI Desemba mwaka jana, zilionyesha katika kipindi cha kuanzia mwaka 2008 hadi 2019, majeruhi 110,679 walipokewa MOI.

Kati yao, waliotokana na ajali za bodaboda ni 59,671, magari 21,711 na ajali zinginezo walikuwa 29,297.

Akitoa mada katika mafunzo hayo, Dk. Nchimbi alisema elimu hiyo endelevu kwa madereva wanaoendesha vyombo vya moto, inaelimisha namna ya kutoa huduma ya kwanza.

Alisema mara nyingi ajali hutokea baada ya dereva kupata tatizo la afya ya akili.

Bingwa huyo anasema kwamba aina ya majeraha ambayo hupata madereva hujumuisha kiuno, miguu eneo la paja na mikono ambayo hushika usukani.

“Ajali za barabarani zinatia hasara taifa, gari linalobeba abiria 30 na hao wote ni wategemezi, akipata ajali hatokwenda kazini, mshahara hatapata, kumbuka nyumbani tumeacha wanaotutegemea,” alionya.

“Huduma kama hamna kwa jamii, uchumi unashuka, magonjwa ya ajali na majeruhi wengi yanachangia kudhoofisha uchumi wa nchi kuliko magonjwa kama kisukari, presha, UKIMWI, TB na malaria.

“Dereva akipata ajali anakuwa hana kitu kingine cha kusaidia kuendesha maisha. Amekatwa mguu au umevunjwa. Hizi ni sababu za kushusha uchumi na utegemezi ngazi ya familia utaongezeka,” alifafanua.

**MIVUNJIKO AINA YAKE**

Bingwa huyo alibainisha kuwa taasisi hiyo katika utafiti iliowahi kufanya, wamekumbana na aina za kipekee za mivunjiko waliyopata majeruhi wa ajali za barabarani, ambayo haijawahi kushuhudiwa wala kurekodiwa kwenye vitabu vya kitabibu nchini.

Alibainisha kuwa kwa siku, MOI hupokea majeruhi wa ajali wapatao 20 na wengi wao huhitaji huduma ya dharura ya upasuaji na kuwekewa vifaa mbadala kama vile chuma.

“Kipindi cha miaka 20 ambacho nimehudumu kwenye fani hii, kuna mivunjiko ambayo sijakutana nayo wala hata kuwapo katika vitabu, unakuta mivunjiko hiyo ndiyo kwanza inaingia kwenye rekodi, kwamba karne nyingi zimepita haijashuhudiwa mivunjiko hiyo katika tiba.

“Ukiangalia katika takwimu unakuta ni mvunjiko unaohitaji kuingia kimataifa na tunaingiza katika vitabu na Tanzania kurekodiwa kwa mivunjiko hiyo.

“Lakini ikumbukwe ni sifa ambayo haipendezi kwa sababu aliyepata jeraha ni ndugu yako, mwendokasi haufai kushangiliwa,” alionya.

**NGUVU ZA KIUME**

Dk. Nchimbi alibanisha kiwango kikubwa cha majeraha eneo la nyonga (kiuno), husababisha matatizo ya uzazi baada ya tiba.

“Wengi hupata mvunjiko wa kiuno ama nyonga ambao unabeba mfumo wa uzazi, haja kubwa na ndogo.

“Tatizo kubwa linalobainika baada ya tiba ya kibingwa kwa majeruhi wa ajali ni kushindwa kushiriki tendo la ndoa.

“Wengi wanakuja wanasema wamepona lakini hawawezi kushiriki tendo. Anaumia kiasi ambacho hata haijawahi kutokea, idadi ya waopata ajali inaongezeka, hivyo ni vyema kuepukwa,” alionya.

**GHARAMA ZA TIBA**

Dk. Nchimbi alisema madhara ya ajali hayaishii katika mwili pekee bali ni tatizo la kisaikolojia na hasara kwa taifa kutokana tiba ya kibingwa anayopatiwa mgonjwa kuhitaji vifaa na wataalamu wabobevu.

“Gharama zilizopo katika sekta ya afya hasa upande wa matukio ya ajali ni pesa nyingi, huku familia zikipata umaskini na kuongeza idadi ya yatima.

“Kinga ni bora kuliko tiba. Mfano kuweka chuma katika mfupa wa paja ni si chini ya Sh. milioni mbili hadi tatu, ambazo kati yake, mgonjwa anachangia Sh. 200,000, pesa nyingine inatolewa na serikali.

“Gharama za matibabu ni kubwa kuliko hata za wagonjwa 10 wa TB, malaria, majeruhi 10 wa ajali waliovunjika vibaya watahitaji Sh. milioni 20 au 30,” alisema.

Dk. Nchimbi aliwataka madereva kuepuka vilevi na uvutaji wa bangi kwa kuwa ni hatari kwa afya ya akili na uendeshaji wa vyombo vya moto.

**LATRA**

Meneja Usalama Barabarani na Mazingira Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), Geoffrey Silanda, alisema madereva kuendesha gari kwa kujiamini kupitiliza na matumizi ya vilevi ni miongoni mwa sababu za ajali za barabarani.

Mkuu wa Ukaguzi wa Magari Tanzania kutoka Kikosi cha Usalama Barabarani, ASP Ibrahimu Samwix, alisema mwendokasi na kitendo cha dereva kutaka kulipita gari ni chanzo cha ajali nyingi na kwamba ajali mbaya zaidi ni magari kukutana uso kwa uso.

# Vigezo vyachuja 120,000 ajira 9,400

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KATIBU Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, ametaja vigezo vitano vilivyowapa ajira 9,475 wataalamu wa afya na walimu wa shule za msingi na sekondari nchini.

Maombi ya ajira hizo yalitangazwa Mei 9, mwaka huu baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kutoa kibali cha ajira kwa walimu 6,949 na wataalamu wa afya 2,726.

Akitoa taarifa hiyo jana jijini hapa, Prof. Shemdoe alisema waombaji wa kada ya ualimu walikuwa 99,583 na wataalamu wa kada ya afya walikuwa 37,437 wakiwamo wenye ulemavu 1,099.

Alitaja vigezo vilivyotumika kuwapata watumishi waliokidhi sifa kuwa ni pamoja na mwaka wa kuhitimu chuo ambapo waombaji waliomaliza mapema zaidi kati ya mwaka 2012 na 2019 walipewa kipaumbele huku mahitaji yaliyopo katika kada husika nayo yakizingatiwa.

Alisema umri wa mwombaji umezingatiwa kwa kutoa kipaumbele kwa waombaji wenye miaka zaidi ya 40.

“Sababu ni kuwa kama hawataajiriwa mapema, wakifikisha miaka 45, hawataweza kuajiriwa tena serikalini kwa ajira ya masharti ya kudumu,” alisema.

Kiongozi huyo alisema waombaji walifungana kwa sifa zilizobainishwa awali, yaani mwaka wa kuhitimu na umri, amepewa kipaumbele mwanamke bila kuathiri uwiano wa asilimia 50.

“Endapo waombaji wamefungana kwenye sifa ya mwaka wa kuhitimu, umri na jinsia basi amepewa kipaumbele mwenye umri mkubwa zaidi kwa kuangalia tarehe ya kuzaliwa,” alifafanua.

Alisema kilichosababisha baadhi ya waombaji kupoteza sifa ni pamoja na kutoweka kwa usahihi viambatisho vyote vinavyohitajika kwa mujibu wa tangazo la ajira na waombaji kutofuata maelekezo ya mfumo wa maombi ya ajira.

“Pia kutofautiana kwa taarifa za mwombaji alizojaza kwenye mfumo wa maombi ya ajira na taarifa zilizopo kwenye viambatisho pamoja na waombaji kuandika taarifa zisizo sahihi kuhusu masomo anayoomba kufundisha na yaliyopo kwenye vyeti mafunzo au hati za matokeo,” alisema.

Prof. Shemdoe alisema baada ya kukamilisha taratibu zote za uchakataji wa maombi, serikali imewapangia vituo vya kazi walimu 3,949 wa shule za msingi na 3,000 wa shule za sekondari na wataalamu wa kada za afya 2,726.

Aliagiza waajiriwa wapya kuripoti kwa Wakurugenzi wa Halmashauri na kufanya kazi kwenye vituo walivyopangwa na siyo katika Makao Makuu ya Halmashauri.

“Mwajiriwa mpya atakayechukua posho ya kujikimu na baadaye asiripoti katika kituo chake cha kazi, alichopangiwa atachukuliwa hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na taratibu,” alisema na kusisitiza waripoti ndani ya siku 14 kuanzia Julai Mosi hadi 14 mwaka huu.

“Wajiriwa wapya wanatakiwa kuripoti katika vituo vyao vya kazi wakiwa na vyeti halisi vya kidato cha nne na sita, vyeti halisi vya kitaaluma vya kuhitimu mafunzo katika kada husika, kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho ya NIDA pamoja na cheti halisi cha kuzaliwa,” alisema.



KUELEKEA SIKU 100 ZA RAIS SAMIA IKULU

# Rais Samia 'ameupiga mwingi'

## •Kila sekta ameigusa kwa namna yake...

**Na Sanula Athanas**

LEO zinatimu siku 100 tangu Samia Suluhu Hassan, aapishwe kuwa Rais wa Tanzania Machi 19, mwaka huu.

Kushika kwake madaraka hayo kumetokana na matakwa ya kikatiba, kwamba Makamu wa Rais ataapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumalizia kipindi kilichosalia kabla ya kufanyika kwa uchaguzi mkuu mwingine pale Rais aliyepo madarakani anapofariki dunia.

Kwa wafuatiliaji wa mchezo wa mpira wa miguu, mchezaji anayeng'ara katika mechi husika, tunasema 'jamaa ameupiga mwingi leo'.

Na hicho ndicho kinachoonekana unapozimulika siku 100 za Rais Samia Ikulu. Tangu aapishwe kushika madaraka hayo makubwa, Mkuu wa Nchi huyo amefanya mambo mengi kwa mustakabali wa taifa. Leo tunayaangazia machache kwa baadhi ya sekta.



Rais Samia Suluhu Hassan, akila kiapo cha kuwa Rais wa Tanzania Machi 19 mwaka huu.. **PICHA: MAKTABA**

**DIPLOMASIA**

Chini ya Rais Samia, serikali imefanikiwa kuimarisha uhusiano wa Tanzania na nchi zingine, kukishuhudiwa ongezeko la misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Huku akibadili baadhi ya viongozi kwenye eneo hilo, yakiwamo mabadiliko ya waziri mwenye dhamana ya ushirikiano wa kimataifa, ni katika kipindi hicho vikwazo 30 visivyo vya kikodi vilifutwa kati ya Tanzania na Kenya.

**UCHUMI**

Katika siku za mwanzo za uongozi wake, Rais Samia aliweka wazi kwamba hahitaji kodi itokanayo na dhuluma, akiwataka watendaji wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kukusanya kodi kwa weledi na kuachana na matumizi ya nguvu katika kudai kodi.

Licha ya uamuzi wake huo ambao yeye alibashiri ungepunguza mapato ya serikali kwa kiwango fulani, TRA imebainisha hali ya makusanyo inakwenda vizuri na hayajashuka.

**UWEKEZAJI, BIASHARA**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2019/20, inabainisha kupungua kwa asilimia 48 ya miradi ya uwekezaji na biashara nchini iliyosajiliwa kwenye Kituo cha Uwekezaji (TIC) katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Kudorora huko kwa miradi pia kumeporomosha ajira kutoka waajiriwa 63,223 mwaka 2015/16 hadi waajiriwa 32,115 mwaka 2019/20.

Kwa kulitambua hilo, ndani ya kipindi hicho cha siku 100, Rais Samia ametilia mkazo suala hilo akiagiza kutengenezwa mazingira rafiki ya uwekezaji na biashara nchini.

Ni katika kipindi hicho kuna miradi mipya imeanzishwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa kiwanda cha bia Dodoma kitakachotumia malighafi ya ndani na upanuzi wa Kiwanda cha Sukari Kilombero, huku tozo na kodi kero kibiashara na uwekezaji zikifutwa.

**UDHIBITI WA MAPATO**

Rais Samia amejipambanua kwamba hana urafiki na mafisadi na wala rushwa.

Katika mwezi wake wa kwanza madarakani, aliagiza kufanyike uchunguzi maalum aliouita 'special kazi' kwenye Benki Kuu (BoT) kufuatilia fedha zote zilizotolewa katika benki hiyo miezi mitatu ya mwanzo ya mwaka huu.

Uchunguzi mwingine umeagizwa na serikali yake ufanyike katika Wizara ya Fedha na Mipango, baada ya kubainika kutumika kitatanishi mabilioni ya shilingi mwezi uliopita.

**USAWA KIJINSIA**

Rais Samia pia ametilia mkazo usawa kijinsia, akilipa nafasi kundi la wanawake ambalo bado liko nyuma katika uongozi na ushiriki kwenye vyombo vya uamuzi.

Wakati wa mkutano wake na kinamama jijini Dodoma, Rais Samia, alilifafanua kwa kina suala hilo na mikakati yake ya kuwainua watoto wa kike, hasa kuwapatia elimu ya sayansi na teknolojia huku akiunda timu kwa ajili ya kumsaidia kuwakomboa wanawake kiuchumi nchini na barani Afrika.

**UTUMISHI**

Ripoti ya CAG ya mwaka 2019/20 iliyowasilishwa bungeni Aprili mwaka huu, ilibainisha kuwapo uhaba mkubwa wa watumishi, hasa kwenye mamlaka za serikali za mitaa, kunakosababisha kushuka kwa ufanisi katika utendaji.

Rais Samia ndani ya siku 100 za uongozi wake ameanza kulifanyia kazi suala hilo, jana tu serikali ikitangaza kuwapangia vituo vya kazi watumishi wapya zaidi ya 9,400 wa kada za elimu (walimu) na afya.

Watumishi wapya hao ni sehemu ya 40,000 ambao Rais Samiaameahidi kuwaajiri katika bajeti yake ya kwanza ya 2021/22.

Ni ndani ya kipindi hicho cha siku 100 za Rais Samia Ikulu, watumishi maelfu wameshuhudia kupanda madaraja na hivyo kuwa na ongezeko katika mishahara yao kuanzia mwezi huu, huku serikali ikiahidi kulipa malimbikizo ya madeni kwa watumishi na watoa huduma (wafanyabiashara).

**UTAWALA WA SHERIA**

Katika uongozi wake, Rais Samia amejipambanua kufuata misingi ya utawala wa kisheria, akizionya mamlaka dhidi ya kadhia ya ubambikaji kesi na kuonea wananchi.

Katika hilo, kumeshuhudiwa ndani ya siku 100 kesi nyingi za uhujumu uchumi na utakatishaji zikifutwa katika mahakama mbalimbali nchini, huku Rais akimsimamisha kazi aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro ili kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zinazomkabili.

**HABARI, MICHEZO**

Katika kuhakikisha kunakuwa na uhuru wa habari nchini, Rais Samia alianza kwa kuagiza kufunguliwa kwa baadhi ya vyombo vilivyofungiwa na serikali huku akiwataka watendaji wa serikali kuvipa ushirikiano vyombo vya habari.

Ni katika siku 100 za uongozi wa Rais Samia, serikali kupitia kwa Waziri Mkuu, imeagiza taasisi za serikali zikiwamo wizara, kulipa madeni zinayodaiwa na vyombo vya habari.

Serikali yake pia imeondoa kodi katika nyasi za bandia ili kutoa msukumo wa uimarishaji wa viwanja vya michezo nchini na kutanua fursa za ajira kwa vijana.

**CORONA**

Virusi vya corona vimeathiri sekta nyingi duniani tangu vilipuke Wuhan, China mwishoni mwa mwaka 2019.

Rais Samia ametilia mkazo kuzingatiwa kwa ushauri na maelekezo ya wataalamu katika kukabiliana na janga hilo na Watanzania kuendelea kumtanguliza Mungu.

**SEKTA YA ELIMU**

Mbali na kuajiri walimu wapya zaidi ya 6,000 ndani ya siku 100 za uongozi wake, Rais Samia ameimulika kwa kina sekta hii.

Serikali yake imelazimika kuongeza bajeti ya ziada ya Sh. bilioni 125 ili kuanza ujenzi wa maboma ya madarasa ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza watakaohitimu kwa mara ya kwanza darasa la saba tangu kuanzishwa kwa Mpango wa Serikali wa Kutoa Elimumsingi Bila Malipo, maarufu Elimu Bure.

Serikali ya Rais Samia pia imelazimika kuongeza bajeti ya nyongeza ya Sh. bilioni 70 ili wanafunzi wote wenye sifa waliokosa mkopo wa elimu ya juu, waupate mwaka ujao wa masomo.

Rais Samia pia amefuta makato yaliyolalamikiwa kuwa ya kinyonyaji katika urejeshaji wa mkopo wa elimu ya juu.

Hapo unazungumzia deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka kuanzia tarehe ambayo mnufaika alianza kupokea fedha za mkopo pamoja na penalti ya asilimia 10 kwa wanufaika wanaoshindwa kuanza kulipa madeni baada ya kumalizika kwa kipindi cha neema cha miaka miwili baada ya kuhitimu masomo yao.

**ULINZI, USALAMA**

Siku za mwanzo za uongozi wake, kulionekana kuanza kurejea kwa matukio ya ujambazi. Alionya alichokiita 'kutikisa kibiriti', akisitiza hali ya usalama mikoani ndicho kitakuwa kipimo kwa makamanda wa polisi wa mikoa.

Katika siku 100 za uongozi wake, neema imewaangukia Jeshi la Polisi na Magereza walioshuhudia kupandishwa vyeo.

Yapo mengi yaliyofanywa na Rais Samia katika kipindi hicho cha siku 100 Ikulu. Hakika 'ameupiga mwingi!'.

HABARI KITAIFA

# ‘Changamkieni fursa za PSSSF’

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, amewahamasisha watumishi wa Kituo cha afya Makole kuchangamkia fursa ya kununua nyumba na viwanja vya makazi, katika mpango unaoendeshwa na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na Benki ya Azania.

Mavunde alisema hayo juzi jijini hapa alipopokea vifaa tiba vilivyotolewa na PSSSF kwa Kituo cha Afya Makole kama sehemu ya maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma. “Ndugu wafanyakazi wa Kituo cha Makole, ninawahamasisha jitokezeni kutumia fursa hii ya kumiliki nyumba na viwanja kama walivyosema wenzetu wa PSSSF, kwa mpango huu wa kulipa kidogo kidogo, ninaamini kila mmoja anaweza kupata anachotaka, hivyo jitokezeni,” alisisitiza Mavunde. Alisema PSSSF kwa kushirikiana na Benki ya Azania wana utaratibu wa kukopesha nyumba zilizojengwa na mfuko na viwanja kwa wanachama wake na wananchi kwa ujumla kwa riba nafuu na masharti rafiki zaidi kwenye soko. “Lengo la mpango huo ni kuwawezesha wanachama na wananchi kumiliki nyumba na viwanja kwa utaratibu wa kulipa kidogo kidogo kwa riba nafuu ya asilimia 10. Bei ya nyumba ni kati ya milioni 36 hadi 61 kutegemeana na ukubwa wa nyumba,” alisema.

Alibainisha kuwa nyumba zinazouzwa zipo katika mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro, Shinyanga, Tabora, Mtwara na Iringa.

Alisema viwanja vipo Ruvuma, Kagera, Tabora, Iringa, Katavi, Morogoro, Dar es Salaam, Rukwa, Lindi na Mtwara. Kuhusu msaada huo, Mavunde aliishukuru PSSSF kwa kuendelea kusaidia kituo hicho ambacho kinatoa huduma kwa watu wengi zaidi wakiwamo watumishi wa PSSSF.

“Msaada huu utakwenda kuleta matokeo chanya kwa wananchi wote. Ninaomba mkifanye kituo hiki kiwe rafiki kwenu kwa kuendelea kutoa misaada mara kwa mara,” alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema wametoa msaada huo ili kuboresha huduma zitolewazo kwenye kituo hicho. “Kama mjuavyo, nia ya serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anapata huduma bora za afya.

“Ili kuhakikisha tunaendeleza azma hiyo, katika maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma mwaka huu, tunachangia vifaa tiba katika kitengo cha kinamama wajawazito na kitengo cha meno kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma za tiba ya meno ikiwamo utengenezaji wa meno bandia,” alisema.

# Waandamana kudai kuajiriwa mgodini

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

VIJANA wanaozunguka mgodi wa dhahabu wa Bulyanhuru wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameandamana wakiwa na mabango kushinikiza wapewe ajira.

Maandamano hayo yalifanyika juzi, vijana hao wakibeba mabango yenye ujumbe mbalimbali wa kutaka ajira ndani ya mgodi huo wa dhahabu.

Hata hivyo, maandamano yao hayo yaliingia dosari baada ya Jeshi la Polisi kuingilia kati na kuwatawanya.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, vijana hao walisema wanaona haiwezekani kuvumilia kuendelea kuishi maisha magumu wakati wanazungukwa na mgodi wenye madini ya dhahabu, huku wakishuhudia wenzao kutoka maeneo mengine wakipata ajira kwenye mgodi huo na kuishi vizuri.

Mmoja wa vijana hao, Kulwa Batromayo, alisema wameamua kuandamana ili kufikisha ujumbe kwa serikali na kwenye mgodi huo.

“Sisi vijana ambao ni wazawa na ni wakazi wa Bulyanhuru, hatunufaiki kabisa na madini yetu ambayo yanachimbwa na mgodi huu.

“Tunaishi maisha magumu sana badala yake watu kutoka maeneo mengine, na sisi tuna uwezo mzuri tu wa kufanya kazi,” alilalamika.

Gradisa Kamugisha, mkazi mwingine wa eneo hilo, alidai kinamama wamekuwa wakinyimwa fursa ndani ya mgodi huo hata kuanzisha migahawa na kwamba nafasi hizo wanapewa watu kutoka Dar es Salaam.

Alisema vijana wanaozunguka mgodi huo wanaishia ‘kuponda mawe’ kwenye migodi midogo ili wapate pesa ya kujikimu kimaisha.

“Hapa mgodini kuna kazi pia za usaidizi, lakini tunaambiwa mpaka tuwe na ujuzi wa miaka miwili hadi mitatu na wakati kazi usaidizi siyo za mtu aliyesoma.

“Kazi wanapewa watu wengine, tunaomba serikali iweke mpango mkakati wa kutoa ajira moja kwa moja kwa vijana wa hapa kupata ajira kwenye mgodi huu,” alisema.

Meneja wa Mgodi wa Bulyanhuru, Zumbi Musiba, alikanusha madai ya kutowaajiri vijana wanaozunguka mgodi huo, akibainisha kuwa asilimia 50 ya vijana walioajiriwa kwenye mgodi wanatoka katika vijiji vyote vinavyowazunguka.

Alisema mgodi huo una uwezo wa kuajiri watu zaidi ya 3,000, lakini ni ngumu kwao kutoa ajira kwa watu wote wanaouzunguka, hivyo wameajiri wachache, tena kwa kuandikiwa barua na wenyeviti wao wa vijiji.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, alikiri kutokea kwa maandamano hayo na kubainisha kuwa jeshi liliingilia kati kuyatuliza na hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kwa sababu vijana walikuwa na lengo la kufikisha ujumbe tu kwenye mamlaka husika.



Rais wa Rotary Klabu ya Dar es Salaam (Mzizima), Wakili Michael Kamazima (kulia), akimvalisha cheni rasmi Rais mteule wa klabu hiyo, Dk. Hawa Banyani, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wapata mbinu usawa kijinsia

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WABUNGE wameshauri mambo kadhaa kufanyika ili kuongeza nafasi ya wanawake kwenye vyombo vya uamuzi ikiwamo kuweka kanuni za uchaguzi zinazomwondoa mgombea anayefanya kampeni za kumdhalilisha mwenzake kijinsia.

Ushauri huo ulitolewa jana jijini hapa kwenye mkutano wa wabunge juu ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi ili kufikia usawa wa 50 kwa 50. Mkutano huo uliandaliwa na Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) kwa kushirikiana na Kituo cha Usuluhishi (CRC) na Young & Alive Initiative (YAI), kwa ufadhili wa Shirika la Kihabari la Femnet. Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ng’wasi Kamani, alisema wanawake wapo tayari kuongoza lakini kuna tatizo wanapokwenda kwenye majukwaa ya kisiasa, hudhalilishwa kijinsia na kuwafanya wakate tamaa au jamii kutowapa fursa ya kuwa viongozi.

Alisema wanawake wengi hujitokeza kugombea lakini vitendo vya udhalilishaji ndivyo vinavyowakatisha tamaa.

“Mwanamke akijitokeza kugombea kuna mambo fulani, anafanyiwa na jamii na kukatishwa tamaa.

“Mimi ninashauri kama wabunge tuangalie namna ya kutunga sheria au kanuni iwekwe ili anayemfanyia mwanamke udhalilishaji wa kijinsia kwenye kampeni, aondolewe kwenye kinyang’anyiro.

“Nimezunguka mikoa mingi kupiga kampeni mwaka jana, kuna jimbo nilipita yule mama aliyekuwa anagombea alikuwa mjane lakini yule mgombea mwenzake mwanamume alikuwa anasema yule mwanamke ni msimbe (amefikia umri wa kuolewa hajaolewa).

“Ni kashfa kubwa sana usukumani, ni moja ya vitu vilimuumiza kwenye kampeni kwa kuwa wanaume walikuwa wanasema hatuwezi kwenda kwenye kampeni ya mtu msimbe wakati yule mama ni mjane,” alisema.

Mbunge wa Chakechake, Ramadhan Suleiman Ramadhan, alisema tatizo lililopo ni utayari wa vyama vya siasa katika kufanya mifumo yake ya ndani iwezesha wanawake kufikia 50 kwa 50.

Mbunge wa Mlalo, Rashid Shangazi, alisema mwanamke ni kiongozi na uongozi wake unaanzia ngazi ya familia.

Mbunge wa Viti Maalum, Aysharose Matembe, alishauri ili kufikia usawa wa 50 kwa 50, watoto wa kike wajengewe uwezo kuanzia shuleni ili kujiamini.

Mbunge wa Viti Maalum, Agness Hokororo, alisema kuna haja ya viongozi wanawake kuwawezesha zaidi wenzao ili kuingia kwenye nafasi za uamuzi. Akihitimisha majadiliano hayo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Wanawake Bungeni (TWPG), Shally Raymond, alisema usawa wa 50 kwa 50 kwa Tanzania utafikia kutokana na kuwa na Rais mwanamke.

Hata hivyo, alishauri wabunge kuzingatia kwamba Tanzania kuingia uchumi wa kati, ufadhili kwenye baadhi ya maeneo utapungua hivyo waangalie namna ya kuishauri serikali kutenga fedha kwa ajili ya mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotetea wanawake.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Rose Reuben, alisema takwimu kwa sasa zinaonyesha asilimia 37 ya wanawake ndiyo wapo kwenye ngazi za uamuzi bungeni.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

HOSEA PATERSON KAJANGE ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 547 CFH – TOYOTA KLUGGER. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: KW/RB/3184/21.

116332902

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hoja za wafanyabiashara zipewe uzito unaostahili

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana aliongoza mkutano wa majadiliano kati ya serikali na wafanyabiashara. Mkutano huo ulioandaliwa na Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ulikuwa wa kwanza akiwa mwenyekiti tangu aliposhika madaraka Machi 19, mwaka huu.

Katika mkutano huo uliofanyika jana Ikulu, Dar es Salaam, jumuiya ya wafanyabiashara kupitia Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), iliwasilisha hoja 17 juu ya mambo ambayo Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Samia, inapaswa kuyafanya kwa lengo la kukuza uchumi na kuboresha mazingira rafiki ya biashara.

Hoja hizo, pamoja na mambo mengine, ni ujenzi wa bandari mpya ya Bagamoyo ambao mpango wake ulisitishwa na serikali ya awamu iliyopita kwa madai kwamba masharti ya mkataba hayakuwa na maslahi kwa taifa.

Wafanyabiashara hao, katika kujenga hoja yao, walisema ujenzi wa bandari hiyo ni muhimu na kwamba kama kulikuwa na upungufu katika mkataba ni vyema ukarejewa au wakatafutwa wabia wapya katika uwekezaji wa mradi huo.

Pia waliweka bayana kwamba hivi sasa kuna mageuzi makubwa katika sekta ya uchukuzi Afrika, hivyo kama Tanzania itaendelea kutegemea bandari ya Dar es Salaam itakuwa nyuma kiushindani kutokana na baadhi ya nchi kama Kenya, Msumbiji na Namibia kufanya upanuzi wa bandari zao.

Kutokana na upanuzi huo, walibainisha kuwa bandari ya Dar es Salaam itakuwa kama kituo cha daladala kwa kuwa meli ndogo pekee zitakuwa zinaingia ilhali kubwa zitakuwa zinatia nanga Mombasa na Lamu nchini Kenya kisha meli ndogo kuleta mizigo nchini.

Jambo la pili ambalo wafanyabiashara waliliwasilisha ni udhibiti hasa ukaguzi wa magari unaofanywa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) nchini badala ya kufanyika kabla ya kusafirishwa kama ilivyokuwa awali. Hatua hiyo, imeelezwa na wafanyabiashara hao kwamba imesababisha kuingizwa kwa magari mabovu nchini, hivyo kusababisha hasara kwa waagizaji.

Wafanyabiashara hao wameshauri kwamba ukaguzi ufanyike na kampuni zinazoteuliwa kabla ya kuanza kusafirishwa na kuingizwa nchini huku TBS ikibaki na jukumu la udhibiti.

Suala la tatu ni uwezeshaji wa kampuni za kizawa kushiriki katika miradi ya kiuchumi na biashara pamoja na kupewa zabuni katika kazi mbalimbali. Hiyo ni kutokana na baadhi ya kazi kama vile za ulinzi, ukusanyaji madeni na uwakala wa forodha kufanywa na taasisi za serikali kama vile SUMA JKT na Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), hivyo kuiacha sekta binafsi kukosa kazi.


Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yameonyesha wazi kwamba yanaweza kufanyiwa marekebisho na kufanyiwa kazi kwa yale ambayo yaliwekwa kando kwa sababu mbalimbali.

Pamoja na Rais Samia kukubali kuwa atazifanyia kazi, hoja hizo za wafanyabiashara ni za msingi, ni vyema serikali ikazichukulia kwa uzito wa kipekee na kuharakisha utekelezaji wake ili kuleta maendeleo ya kweli na endelevu kupitia ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Ni ukweli usiopingika kwamba katika mazingira ya sasa ya uchumi wa soko, sekta binafsi inapaswa kupewa kipaumbele huku serikali ikibaki na jukumu kuu la udhibiti na kuweka mazingira rafiki katika biashara na uwekezaji pamoja na kutunga sheria na sera ambazo zitatoa vivutio katika ukuaji wa uchumi.

Sambamba na hilo, ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, kutokana na ushindani uliopo duniani, Afrika ikiwamo, kama ilivyobainishwa na wafanyabiashara, unapaswa kupewa umuhimu wa kipekee. Katika hili, siasa zinatakiwa kuwekwa kando kwa maendeleo endelevu ya uchumi wa nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Tahadhari ya wizara ya afya dhidi ya corona si ya kuzembea

**SASA** ni wazi kwamba kila Mtanzania anatakiwa kuchukua tahadhari zote ambazo zimekuwa zikielekezwa na wataalamu wa afya, kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa hatari wa corona.

Hii ni kutokana na wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania kuwakumbusha kutopuuza ugonjwa huo, kwa kuwa imeanza kuona viashiria vya kutokea kwa wimbi la tatu la mlipuko wa corona nchini.

Mkurugenzi wa Kinga wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk Leonard Subi, anatoa maagizo kadhaa ikiwamo kuwataka Watanzania kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Mbali na maagizo hayo, mengine ni kunawa kwa maji tiririka na sabuni, kutumia vitakasa mikono kila mara kwa ajili ya usalama wao, kwa kuwa viashiria vya kutokea kwa wimbi la tatu la mlipuko wa corona nchini vimeanza kuonekana.

Wizara imechukua hatua hiyo kutokana na taarifa za ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa huo zinazofanywa na wizara na mwingiliano kati ya Watanzania na watu wa mataifa mengine.

Maelekezo hayo ya wizara yenye dhamana ya afya za Watanzania, yanafaa kuzingatiwa, kwa kuzingatia kuwa, afya njema ni ya muhimu, hivyo kila mmoja wetu hana budi kujitahidi kulinda afya yake.

Ikumbukwe kwamba, mtu akiugua, hakuna wa kumsaidia kubeba ugonjwa wake, kwani ataugua mwenyewe na maumivu ni yake mwenyewe na hata akifariki atapelekwa kaburini mwenyewe.

Kwa maana hiyo, ni muhimu kwa kila mmoja wetu kuzingatia tahadhari zote zinazotolewa na wataalam wa afya kuhusu njia ya kujikinga na ugonjwa huo hatari ili kuendelea kulinda afya zetu.

Wizara inabainisha kuwa idadi ya wagonjwa wanaopatikana na vizuri vya corona barani Afrika imeongezeka ndani ya wiki tano mfululizo zikiwamo nchi zinazopakana na Tanzania, na kwamba maambukizi yanaongezeka maradufu kuliko ilivyokuwa wimbi la pili.

Kuna msemo wa Kiswahili usemao; 'Mwenzako akinyolewa, zako tia maji', hivyo wakati majirani zetu wakiendelea kuumizwa na ugonjwa huo, Watanzania hatuna budi kuchukua tahadhari zote za kujinga nao.

Lakini pamoja na maelekezo ya wizara yenye dhamana ya afya zetu, bado kuna sehemu nyeti ambayo ninaona kuwa kuna haja ya kuirekebisha ili kusaidia umma wa Watanzania kuepusha maradhi hayo hatari.

Hii inahusu usafiri hasa wa daladala, kwani abiria wamekuwa wakijazana kupita kiasi jambo ambalo ni hatari kwa afya zao hasa wakati huu dunia inaposumbuliwa na ugonjwa huo.

Mwaka jana, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini nchini (LATRA), ilitoa maelekezo mbalimbali kwa wadau wa usafirishaji zikiwamo daladala kuhakikisha wanabeba abiria kulingana na idadi ya viti.

Lengo lilikuwa ni kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona ambavyo viliingia nchini na kusababisha serikali kufunga shule zote ili kuepusha wanafunzi kukumbwa na maradhi hayo.

Wakati huu ambao wizara imetoa tahadhari la maelekezo, ni vyema wadau wa usafirishaji wa abiria hasa ndani ya jiji la Dar es Salaam ambalo lina shida ya usafiri wakachukua hatua za kuongeza usafiri huo.

Tunakumbushwa kutopuuza ugonjwa huo, kwa kuwa wizara husika imeanza kuona viashiria vya kutokea kwa wimbi la tatu la mlipuko wa corona nchini, lakini msongamano wa abiria ndani ya daladala ni ule ule wa miaka yote.

Ninadhani wakati muafaka kwa wakazi wa jiji la Dar es Salaam kuongezewa usafiri wa umma ili waache mtindo wa kubanana ndani ya daladala au mwendokasi, hali ambayo ni hatari kwa afya zao hasa kipindi hiki cha corona.

Pamoja na hayo, elimu juu ya kujikinga na virusi vya corona iendelee kutolewa ndani ya vyombo vya usafiri kwa kutumia redio na runinga zilizomo ndani ya vyombo hivyo badala ya kupiga muziki wa kizazi kipya tu.

Kwa wale wanaotumia usafiri wa daladala, watakubaliana nami kwamba, asilimia kubwa zinapiga muziki huo ambao nyimbo zake nyingi hazina mafunzo bali ni kuburudisha tu.

## SAFU

### KWA MASLAHI YA TAIFA

# Baadhi ya Majaji, Mahakimu hawana jicho la haki!



Na Pascal Mayalla

**Mimi nikaanza kuifuatilia "Kesi ya Mauaji Mwanza" kwenye gazeti la Mzalendo kila Jumapili, Baba alikuwa anatetewa na Wakili Murtaza Lakha, kati ya washtakiwa wote, ni baba yangu pekee ndio alinasuka, kutokana na umahiri wa wakili Lakha, wengine wote walifungwa vifungo virefu.**

BAADA ya makala kuhusu Ofisi ya DPP, wiki hii, naugeukia Mhimili wa Mahakama.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati akiwaapisha majaji wapya 28 wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani, alisema na hapa ninanukuu

"Tatizo la ucheleweshwaji wa kesi katika mahakama zetu bado lipo, kama mnavyosema wanasheria haki inayocheleweshwa ndio haki inayokataliwa, hivyo ni imani yangu kuwa baada ya upatikanaji wa majaji hawa ucheleweshaji wa kesi mahakamani utapungua na hatimaye haki kupatikana kwa wakati," alisema Mhe. Rais Samia.

Rais Samia akaendelea kwa kuitaja Ibara ya (107) A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa mamlaka ya utoaji haki ni mahakama, "hivyo jukumu lililopo mbele yenu ni kubwa sana, basi ni vyema mkatekeleze majukumu yenu mliyopewa kwa uaminifu, mkaongoze vyema na mkaongozwe na utu na nafsi zenu katika kuwatumikia wananchi," mwisho wa kunukuu.

Kwa upande wake, Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof. Ibrahim Hamis Juma alimshukuru Mhe. Rais kwa uteuzi wa Majaji hao wapya huku akiwa na imani kuwa idadi hiyo italeta mabadiliko makubwa ambayo yataonekana mara moja.

Jaji Mkuu, Prof. Juma alisema "Mhe. Rais napenda nichukue fursa hii kukushukuru kwa kutupatia Majaji hawa, idadi hii itasaidia kupunguza mzigo wa mashauri kwa majaji waliopo na hivyo kusaidia kuleta mabadiliko ambayo yataonekana mara moja," alisema Mhe. Jaji Mkuu.

Prof. Juma, aliendelea "Mhe. Rais idadi ya Majaji inapanda na kupungua kulingana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kustaafu kwa Majaji pamoja na wengine kupangiwa majukumu mbalimbali, hivyo bado tunaomba kuendelea kupatiwa kadri nafasi zinapopatikana ili kuendelea kutoa huduma ya haki kwa kuwa wananchi wengi kwa sasa wanafahamu haki zao na hivyo kufungua kesi kwa wingi," alieleza Jaji Mkuu.

Kwa vile hoja yangu ya makala hii ni kuangazia uwezo mdogo wa baadhi ya Majaji na Mahakimu wetu, kutokuwa na jicho la ndani, lenye uwezo wa kuona haki, kunakochangia ucheleweshaji wa kesi na ukosefu wa haki, naomba kutoa historia fupi ya maisha yangu na jicho la ndani.

Mimi nimezaliwa katika familia ya watumishi wa serikali kwa baba na mama, Baba Mzee Andrew Mayalla (RIP), akihusishwa na ile kesi ya mauaji Mwanza ya 1976. Enzi za Nyerere, mtumishi wa umma ukistaafishwa kwa manufaa ya umma, breki ya pili ni kurejeshwa kijijini, hivyo tukarejeshwa kijijini usiku kufuatia kesi hiyo. Baba yetu mdogo mzee Mateo Kasanga, akatufuata kijijini mimi na dada yangu Maria, na kutuleta jijini Dar es Salaam kuishi na familia yake.

Mimi nikaanza kuifuatilia "Kesi ya Mauaji Mwanza" kwenye gazeti la Mzalendo kila Jumapili, Baba alikuwa anatetewa na Wakili Murtaza Lakha, kati ya washtakiwa wote, ni baba yangu pekee ndio alinasuka, kutokana na umahiri wa wakili Lakha, wengine wote walifungwa vifungo virefu. Toka wakati huo, nikaanza ku 'develop interest' ya kuwa kama Lakha ili nisaidie watu kupata haki mahakamani.

Familia ya Mzee Kassanga ilikuwa na watoto sita ukijumlisha na watoto wawili, tunakuwa watoto wanane, ni familia kubwa. Ukitokea wizi wowote, udokozi, automatically unajihisi unahisiwa ni wewe, maana kabla ya ujio wenu hakukuwa na wizi wala udokozi. Kuna siku usiku mama K, alisahau fedha mezani, asubuhi akakuta zimepungua, kuna mtu amedokoa!. Wote hatujui ni nani, Baba alishika fimbo, na watoto wote tuliitwa, na kuambiwa tutachapwa wote hadi tumtaje aliyedokoa. Kwa vile hakuna aliyemuona, wakubwa wote tulikula mboko!.

Baada ya kula bakora, sisi wanaume tuliambiwa "msilie lie kama wanawake", hivyo unajikaza, lakini usiku nikakumbuka nimepigwa bila kosa, nikajikuta nalia sana, iweje akose mmoja, halafu tuadhibiwe wote bila hatia?.

Baadhi ya adhabu, nikaanza ku note huku wengine tunasosoneka kuonewa, kuna mwingine amelia kidogo tu, akanyamaza na kuanza kutucheka. Nikamwambia mama K, aliyefanya kitendo hicho ni fulani. Mama akaniuliza ulimuona, nikasema sikumuona, ila najua tu ni fulani. Nikaulizwa umejuaje, nikasema najua tu. Akaulizwa akakataa.

Tukiwa shule, mwenzetu kila saa anatafuna kitu, mara big G, mara mihogo, mara kashata, karanga, kila nikumuuliza anasema amenunuliwa na rafiki zake. Nikamuuliza mmoja wa marafiki zake, akasema ni fulani kaja na hela nyingi ananituma mimi ninunue na kugawia wengine. Hiyo ikapita.

Siku nyingine tena kukatokea udokozi tena, tukaitwa wote, baba fimbo mkononi kama kawaida msiposema, wote tutakula mboko. Baada ya kuwatazama wote usoni, wengine wote wanaogopa kuchapwa, mmoja wetu amekauka tu, huku hana wasiwasi wala haogopi. Nikanyoosha kidole na kusema ni fulani. Akaruka, mama akaniuliza ulimuona, nikasema hapana, akasema si nilikukataza kumsingizia mtu bila ushahidi?.

Baba akaruhusu niseme ni kwanini nimesema ni fulani, nikasema sisi wengine wote tunaogopa, mwenzetu hana wasiwasi, Nikaruhusiwa kuthibitisha, nikaomba kumsachi, huwezi amini, niliibua fedha ya noti imesundwa kati kati ya daftari!. Mhusika aliruka kuwa hajui imefikaje, nikageuziwa kibao ni mimi!. Ikawa likitokea tukio, naitwa kuendesha uchunguzi na nikaanza kuitwa Inspecta Pasikali.

**Tukutane wiki ijayo, kuendelea na simulizi hii.**

### MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Wabunge wetu muwe na kiasi basi!



Na Joseph Kulangwa

**Juzikati nikasikia mbunge akilalamikia mshahara akisema ni mdogo, akisema posho inayolipwa ni kiduchu haimtoshi, akataka alipwe kama mabunge mengine yakiwamo ya Afrika Kusini na Kenya, mbunge wetu akataka alipwe kwa dola ya Marekani!**

NI kwa kuwa tu Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuendeleza na kukamilisha miradi ya kimkakati, na ndiyo sababu Mwigulu Nchemba akaja na mapendekezo ambayo kwa kweli ni vunja mgongo, lakini hakuna namna.

Isingekuwa hivyo na ningekuwa na uwezo, ningemwambia Mwigulu ependekeze hizo fedha zitakazopatikana kwenye laini na miamala ya simu, na kwenye kodi ya majengo kupitia LUKU, ziitishe uchaguzi mkuu mpya wa wabunge tu.

Kila nikikaa na kusikiliza wabunge wetu, najiwa na wazo kama lililomjia Rais Samia Suluhu Hassan wakati mmoja kuwa wanademka, wanajadili wakati mwingine mambo ambayo ukiwaangalia usoni hawafanani nayo!

Kuna wakati nikaacha tu kusikitika, kwa sababu hata baada ya Rais kuwaambia wanademka, ndipo kudemka kukazidi. Nikakumbuka siku moja kuna mtu aliniambia ukiendelea kumfokea mwanao kuhusu kosa fulani hataliacha.

Juzikati nikasikia mbunge akilalamikia mshahara akisema ni mdogo, akisema posho inayolipwa ni kiduchu haimtoshi, akataka alipwe kama mabunge mengine yakiwamo ya Afrika Kusini na Kenya, mbunge wetu akataka alipwe kwa dola ya Marekani!

Akasema tena, aliomba ubunge kwa ridhaa yake kabisa tena kwa moyo mweupe. Nikajiuliza, hakujua kuwa anakwenda kupokea mshahara mdogo? Hakujua kabisa kwamba anakwehda kupokea mamilioni ya kodi ya Mtanzania ambayo kwake ni madogo?

Mbunge wetu huyu, ambaye anataka kutwambia kuwa huko alikotoka, huko anaowawakilisha wanalipwaje? Wana kipato gani hapo Watanzania waliojilawa asubuhi kufoleni kumchagua, wana mapato makubwa kiasi gani?

Ndiyo sababu mimi husema kila siku, hivi kwa nini hii Katiba mpya isiharakishwe, ili iwe na kipengele kisemacho ubunge ni kujitolea? Yaani ufikapo mkutano wa ubunge, ili kwenda Dodoma yapelekwe mabasi au treni mikoani kuwakusanya na kuwaleta Dodoma.

Wakiwa Dodoma walale hata katika chuo kimoja hivi bwenini, wapande daladala, ndipo wajue usiri wa matatizo ya wananchi, na hapo ndipo waanze kuomba mamilioni ya kujikimu, huku wakitetea wananchi waliowachagua kuingia mjengoni.

Hivi mbunge akilalamika, kuwa mshahara na posho wanazolipwa hazitoshi, mkulima ambaye analima kwa jasho na hatimaye kukosa soko asemeje? Vijana waliohitimu vyuo na kurudi mitaani kusaka ajira ambayo haipo wafikirieje?

Yaani badala ya kumtoa nje mbunge aliyevaa tofauti na kanuni zinavyotaka, ni vema mbunge kama huyu atolewe nje akafikirie wananchi wake walivyo, ndipo arudi bungeni, aone kama inafaa kuomba marupurupu au kusaidia wananchi masikini.

Wakati naiandika hii, kuna mtu sijui kaniona, akanipenyezea hii ambayo sina uhakika nayo vizuri labda wajuvi watanisaidia, eti mbunge wa Tanzania analipwa mshahara wa Sh milioni 12 kwa mwezi, eti na posho ya kikao Sh. 340,000 kwa siku!

Mheshimiwa sana mbunge wetu anasema hakuna kitu hapa, na kwamba alitarajia kitu kikubwa zaidi ya hapo lakini hivi vijisenti vya mboga, vimilioni kumi na mbili kwa mwezi ni kitu gani kwake. Anataka Serikali iongeze. Sikatai kama ipo wapewe tu, tufanyeje sasa sisi!

Nikifikiria sifa ya kuwa mbunge, nguvu inaniishia kabisa. Ujue kusoma na kuandika tu. Mshahara Sh. milioni 12 na posho hujasema! Madaktari mpo? Walimu je? Askari? Wauguzi je? Mtasemea wapi?

Mara nyingine, ninaposikia ukakasi kama huu, hubaki kufikiria kwa nini tuwe na Bunge? Badala yake tuwe na kamati ya wataalamu wasomi wawe wanatutungia sheria ili tubane matumizi, au kama lazima tuwe na wabunge wa kuchaguliwa, basi wawe wa mikoa. Kila mkoa mbunge ili tupunguze matumizi.

Ndiyo, tufanye hivyo, ili fedha tutakazookoa, tuzipeleke kwenye miradi ya kimkakati. Hivi nini kitaishinda hiyo kamati, kukaa na kuona hili linafaa hii halifai na kuligagadua kisomi, na kuja na sheria badala ya hii ya wangapi mnaafiki, semeni ndiyo na wanaoafiki wameshinda!

Waheshimiwa wabunge tusigeuke wana Tumbo Street, hebu tufikirie maisha ya wapiga kura vijijini na mijini, hali ni mbaya, nyie wenyewe mmepitisha bajeti ya kuwaparura kwenye laini na miamala, kwenye majengo na vingine, sasa mnataka zilipe posho badala ya kuwasaidia!! Tufikirie basi angalau eh!

**Alamsiki!**

SAFU

## KONA YA UKWELI

# Tubuni miradi, tusisubiri uteuzi



Na Thobias Mwanakatwe

RAIS wa Awamu ya Sita, Samia Suluhu Hassan, hivi karibuni alitangaza mkeka wa zaidi ya wakuu wa wilaya 100.

Uteuzi uliofanywa na Rais Samia ni mwendelezo wa kuisuka serikali yake ili anaowateua wamsaidie katika harakati za kuwaletea wananchi maendeleo.

Inapofikia wakati Rais anaunda serikali yake kwa kuteua mawaziri, wakuu wa mikoa na wilaya, unakuta wanasiasa na wasomi na wananchi wa makundi mbalimbali kila mmoja anatolea macho uteuzi huo akitegemea pengine atakuwamo katika orodha, marufu kama mkeka kama unavyoitwa siku hizi.

Mfano wa karibuni baada ya taarifa rasmi ya uteuzi wa wakuu wa wilaya kutoka hadharani, kumekuwa na miluzi mingi kutoka kwa wanaharakati kwenye mitandao ya kijamii, wanachama na wafuasi wa vyama kama Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia Umoja wa Vijana UVCCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Baadhi ya wanachama wa CHADEMA, hususani vijana, wamekuwa wakiwabeza vijana wa UVCCM kuwa licha ya kwamba wamo ndani ya chama tawala na kuwa mstari wa mbele kukinadi chama chao, bado hawapewi nafasi kwenye uteuzi na badala yake wanateuliwa vijana kutoka vyama vya upinzani hususani waliokuwa CHADEMA kabla ya kuunga juhudi na kurejea CCM.

Binafsi, nimekuwa nikijiuliza huu utamaduni wa malumbano kwa wanasiasa kuhusu uteuzi umetoka wapi, mbona huko nyuma mambo kama haya hayakuwapo.

Nadhani tusimchoshe Rais kwa malumbano yasio na tija kwa nchi. Rais Samia aliweka wazi mapema kwamba katika uteuzi wake kunda serikali atakuwa anachanganya hata wapinzani ili mradi tu wawe na sifa zinazitakiwa.

Wanaozusha hoja hizo zisizo na msingi, wanashindwa kufahamu kuwa anachokifanya Rais Samia ni kutengeneza safu ya viongozi watakaoweza kumsaidia katika kuleta maendeleo, hivyo hakuna chama wa vijana wenye kusema wao ndio wana hatimiliki ni lazima wateuliwe, hawajielewi.

Kimsingi, katika hili naona kabisa 'Something is wrong somewhere'. Hivi ni nani aliyewahi kusema nafasi za Ma-DC ni za UVCCM au CHADEMA?

Tunaposema UVCCM ni taasisi ya kulea viongozi wa leo na kesho, isitafsiriwe kama taasisi ya kuandaa wakuu wa wilaya au viongozi wa kuteuliwa peke yake. Tunahitaji UVCCM itupe viongozi wakubwa wa mashirika ya umma, asasi za kiraia na mashirika binafsi, si ukuu wa wilaya pekee.

Ndani ya CCM kama ilivyo CHADEMA na ACT, hakuna wanachama wa daraja la kwanza wala daraja la pili. Wote ni Wana CCM. Mfano Edward Lowassa alihamia CHADEMA akapewa nafasi ya kugombea Urais, Frederick Sumaye, Lazaro Nyalandu na wengine wakawa viongozi wa Kamati Kuu ya CHADEMA.

Pale ACT kwa Zitto aliendа Benard Membe akawa 'top leader' ndani ya wiki moja. Kule Zanzibar Maalim Seif alitoka CUF akapewa nafasi ya kugombea urais moja kwa moja. Tuseme wote waliokuwa CHADEMA na ACT hawakuwa na uwezo wa kugombea nafasi hizo hadi wana CCM ndio wakawa tegemeo la vyama hivyo?

Tujiulize, kuna mwanachama wa CCM aliyetoka CHADEMA au ACT ambaye kwa sasa ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM? Au kuna aliyetoka upinzani akapata nafasi ya kugombea urais CCM? Tuelewеshane hapo.

Mambo ya uteuzi yaacheni kwa Rais, hata kama mpigadebe angeteuliwa kuwa DC sioni tatizo ili mradi atatekeleza Ilani ya CCM ambayo ni serikali ya chama kilichopo madarakani.

Nasema tuache siasa zisizo na maslahi. Nafasi za ukuu wa wilaya si mali ya waliokulia UVCCM wala CHADEMA. Ni mali ya Watanzania wote kupitia makundi mbalimbali wanaotosha katika nafasi hizo.

Lakini kinachooenekana hadi watu wapigane vikumbo katika uteuzi wanadhani kuwa akishapewa cheo basi ameshaukata kimaisha. Nadhani hizi ni fikra potofu sana. Hivi sasa kuna maelfu ya vijana wasomi wenye madigrii wako mitaani na wao pengine wanasubiri wateuliwe. Huu ni ujinga uliovuka mipaka.

Kama wako wasomi wa aina hiyo, nadiriki kusema wazazi wao waliharibu hela kuwasomesha. Nilitegemea msomi baada ya kumaliza tu masomo yake, abuni mradi ambao utakuwa unamwongezea kipato badala ya kumsubiri mama (Rais) amteue kuwa DC au RC.

Mfano siku moja nilikuwa naangalia taarifa ya habari kwenye luninga nikamsikia kijana mmoja msomi ameamua kuanzisha mradi wa kufuga panya wekundu ambao wanampatia kipato. Kijana kama huyu hawezi kusubiri kuteuliwa ameshajiongeza.

**Mungu ibariki Tanzania**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# KUISHI MBALI NA MWENZI HUATHIRI USTAWI WA FAMILIA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka 0744000066

WATU ni rasilimali muhimu mahali pa kazi. Bila rasilimali watu, hakuna taasisi, shirika, kampuni au serikali. Taasisi zimeundwa na zinafanyakazi kwa njia ya watu. Mafanikio yoyote mahali pa kazi yanategemea watu. Kwa hiyo, watu ni chachu ya mafanikio katika maeneo ya kazi.

Waajiri makini huwekeza katika rasilimali watu kwa kuwajengea uwezo na kuhakikisha watumishi wana furaha mahali pa kazi. Furaha ni kichocheo cha kufanya vizuri. Furaha inapokuwapo, nafsi ya mtu huburudika. Ni vigumu mtumishi asiye na furaha kutoa huduma bora.

Furaha inapokosekana kwa mtumishi huathiri utendaji wake wa kazi na kupunguza uzalishaji; huondoa hali ya kujithamini (personal value), kujiamini (confidence), huvuruga uhusiano wake na watu wengine; hukosa hamasa (motivation) na kusababisha hasara mahali pa kazi.

Upangaji wa vituo vya kazi na uhamisho wa watumishi usiojali ustawi wa familia, huchangia kuondosha furaha ya mtumishi mahali pa kazi. Ninapozungumzia familia katika makala hii nina maana ya baba, mama na watoto. Tunashuhudia leo baadhi ya watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao. Kwa mfano; unakuta kituo cha kazi cha mume kiko Pwani huku kituo cha kazi cha mke kikiwa Kigoma au mume anaishi Njombe na mke anaishi Arusha.

Kwa namna yoyote ile, umbali wa jinsi hii hauwezi kuiacha familia salama. Watumishi wa umma ni wahanga zaidi katika suala hili kuliko watumishi wa sekta binafsi. Wengi wao kazi zimewatenga na familia zao.

Kitendo cha mume au mke kuishi mbali na mwenzi wake ni changamoto kubwa na mtihani mzito. Mara nyingi hali hii imeleta vishawishi na kuathiri uhusiano wa wanandoa wengi kwa sababu ya matatizo yanayozalishwa na umbali. Umbali na hali ya upweke vimechochea baadhi ya wanandoa kuanzisha uhusiano mpya nje ya ndoa ikiwa ni sehemu ya kufidia pengo la umbali. Waathirika wakubwa katika hali hii huwa ni wanawake na watoto.

Uhusiano huu ukiishakolea na kuota mizizi, husababisha mwanandoa kupoteza mvuto na thamani ya mwenzi wake. Hali hii hutengeneza mazingira ya migogoro isiyo ya lazima katika ndoa. Baadhi ya ndoa zimebaki kuwa za heshima tu na kupoteza uhalisia wake. Athari zake ni kubwa kwa wanandoa wenyewe na watoto waliozaliwa katika ndoa hizo.

Wako wanandoa ambao wamevurugwa, wamejeruhiwa nafsi na ndoa kuvunjika kwa sababu ya kuishi mbali na wenzi wao. Wanandoa wanapoishi huyu huku na huyu kule huongeza gharama za maisha, hali ambayo huathiri tabia na mienendo yao. Umbali husababisha msongo wa mawazo ambao huathiri afya ya akili na mwili; hupunguza kiwango cha mshikamano wa wanandoa, mvuto, upendo na joto la ndoa.

Mume na mke wanapoishi mbalimbali huathiri watoto kisaikolojia na kimakuzi kwa sababu ya kukosa malezi ya wazazi wote wawili. Wako watoto ambao wamewachukia wazazi wao na kupoteza mvuto na baba au mama au wote kwa pamoja kwa sababu ya kuhisi kutokupendwa, kupuuzwa na kutelekezwa. Malezi mabaya ya watoto huchangia mmomonyoko wa maadili katika jamii.

Natambua kuwa utumishi ni popote na kwamba mazingira ya kikazi kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kazi hulazimu mume au mke kuishi mbali na familia yake.

Hata hivyo, upo umuhimu mkubwa kutafakari kwa makini na kulipa uzito unaostahili suala hili kwa kuzingatia kuwa wako watumishi wanandoa waliopangwa vituo vya kazi lakini hawana furaha ya kazi na maisha.

Ufanisi wa utendaji wao wa kazi umeshuka na kuleta athari mahali pa kazi. Hali hii hujitokeza kwa kuwa mtumishi anatumia muda wake mwingi zaidi kufikiri kuhusu familia na matatizo ya nyumbani kwake kuliko kazi.

Kwa kuzingatia mazingira halisi wanayokutana nayo baadhi ya watumishi wanandoa wanaoishi mbali na familia zao, natoa ushauri kwa Serikali yetu sikivu kuchukua hatua za makusudi ili kurekebisha hali iliyopo sasa. Ni muhimu zitungwe sheria na kanuni zenye lengo la kuweka utaratibu mzuri zaidi utakaolinda ndoa na ustawi familia kwa madhumuni ya kuongeza tija na ufanisi kazini. Mwanandoa anayetamani kuishi mbali na mwenzi wake atakuwa anatafuta matakwa yake.

Ndoa ni kitovu na msingi wa familia, jamii, taifa na maendeleo. Msingi wa ndoa ukiyumba, kila kitu kitayumba. Kazi zitayumba, ustawi wa familia utayumba, jamii itayumba, taifa litayumba na maendeleo yatayumba kwa sababu ya kukosekana kwa nguvu kazi yenye utulivu na amani. Furaha na amani ya mtumishi ni chachu ya mafanikio mahali pa kazi na maendeleo ya taifa.

Mungu alianzisha ndoa ili mume na mke waishi pamoja kwa furaha. Mafanikio na baraka katika kazi zetu huanzia nyumbani. Mafanikio na baraka hizi hudhihirika pale ndoa zinapokuwa imara. Nyumbani kukiwa vizuri kuna uwezekano mkubwa kazini kukawa vizuri pia. Kazi zipo ili kuleta furaha na siyo kuleta upweke na maumivu. Kwa hiyo, Kazi zisiondoe utu na thamani ya familia. Mungu ibariki Tanzania.

- **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishughulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066].**

# MAISHA

JUNI 27, 2021
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Ukurasa 14

## Vyakula vya kupunguza unene



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Hivi ndivyo unapaswa kuandaa chumba cha mtoto



## HARUSI

Ukurasa 12




**MUSTAFA HASSANALI**

# Mbunifu wa mavazi anayetamani kuona Tanzania inakuwa kinara

Ukurasa 14


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| K | I | F | A | R | U |
| A | ■ | ■ | ■ | A | ■ |
| A | R | I | ■ | I | ■ |
| ■ | O | ■ | S | A | A |
| ■ | Z | ■ | ■ | ■ | Y |
| S | I | M | I | K | A |

## AMSHA AKILI





## TOA TOFAUTI 5




## WATOTO

# PAKA RANGI




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
MIA, ONA, KOO, ADA,
NINI, MOSI, TIBIKA, KALAMU

## CHEKA



Alichokifanya daktari

HIZI ndizo sheria ya mpira wa chandimu mitaa ya uswahilini.

**1.** Mwenye mpira Lazima acheze ata kama hajui mpira
**2.** Dogo mnene Lazima awe golikipa
**3.** Mwenye mpira ataamua nani acheze na nani asicheze
**4.** Kama haujashiriki kufuma mpira unaweza usipate namba
**5.** Ukichaguliwa mwishoni ujue uwezo wako ni mdogo kuliko wote
**6.** Mwenye mpira akikasirika mpira umeisha
**7.** Inaruhusiwa kubadili golikipa kama ikitokea penati na baada ya apo ataendelea kudaka yule yule
**8.** Mechi itaisha pale giza linapoingia
**9.** Wale ambao wamekosa namba kazi yao ni kufata mpira ukitoka
**10.** Yule mtaalam wa soka huwa hakosi namba.

**SWALI**
Kobe anaishi kwa muda wa miaka mingapi? Ukiikumbuka lazima utabasam!

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unatumiaje wakati wako katika maisha?

***KARIBU** tena msomaji wangu katika safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo hebu tujadili 'wakati', eneo ambalo watu wengi hawaelewi kama limebeba sehemu kubwa sana ya hatima ya maisha yetu.*

NENO wakati (nyakati), katika kamusi ya Kiswahili sanifu limetafsiriwa kama muda, majira. Hata katika maandiko ya Mungu neno hili limeainishwa vyema linavyoweza kutumika.

Kwamba kwa kila jambo kuna majira yake na wakati kwa kila kusudi chini ya mbingu. Kwa mfano, kuna wakati wa kulia na wakati wa kucheka, wakati wa kupanda na wakati wa kuvuna, wakati wa kupenda, wakati wa kuchukia, wakati wa vita na wakati wa amani.

Kuna wakati ambao adui humfanyia mtu vita wakati wa amani. Yaani haangalii kuna amani au la, yeye ni vita tu. Kuna mbinu ambazo adui hutumia hata kwenye majira. Anaweza asikupate kwenye maeneo mengine, lakini akahakikisha anakupotezea majira yako ya kufanya kitu sahihi.

Adui anaweza kuona vitu vyote umeshinda. Umepata nafasi nzuri iwe ni cheo na kadhalika. Lakini kitu atakachokupiga nacho ni kuhakikisha kuwa anakupindisha kwenye majira.

Watu wengi kwa sababu ya kutofanya mambo kwa majira na wakati sahihi, wamejikuta wanapata gharama kubwa sana huko mbele ya safari. Na wanatumia nguvu kubwa sana kwa sababu kipindi cha kwenda kupanda wao wamelala. Kipindi cha kuvuna, wao ndio wanakwenda kupanda. Ni ngumu sana mtu wa aina hii kufanikiwa. Hapo adui anaweza kutumia nafasi hiyo kukubadilishia saa au muda.

Yako majira ulipaswa upate kitu kizuri asubuhi lakini adui atakufanya uwe na uvivu fulani ili uchelewe ule muda wa kukutana na kile kitu kizuri. Ni takriban saa moja tu lakini tayari ameshavuruga faida ya wiki na hata mwezi.

Mpenzi msomaji, kuna mtu atafanya uzembe mdogo sana kwa kupoteza dakika mbili au hata tano, kumbe muda huo ndio ulikuwa akutane na mtu sahihi aliyebeba baraka zake.

Siri ambayo anatumia adui ni kwamba anaweza kukuachia kwenye mambo mengine lakini kwenye eneo la majira, kufanya jambo kwa wakati, hapo ataanza sana kushindana nawe. Ndiyo maana utaona mtu anapoinuka kimafanikio hupata upinzani mkali sana.

Yako mambo unapaswa kujiuliza mapema sana; kwamba hivi kipindi hiki ambapo una nguvu, iwe ni kijana au nani, una nguvu ya kufanya jambo, je, unazitumia hizo nguvu kufanya nini?

Kuna majira ambayo unajikuta unafanya kazi nzuri, umeajiriwa na unalipwa mshahara mzuri, hamna shida maisha ni mazuri kabisa. Lakini je, huo mshahara unaufanyia nini? Tatizo si kupata nafasi nzuri na kulipwa vizuri bali kile ambacho unafanyia huo mshahara.

Adui anaangalia kile unachokifanya mara baada ya kupata ile nafasi. Yupo tayari afanye vita yoyote kuhakikisha anakupindisha usifanye chochote. Matokeo yake unashangaa upo pale pale. Yule anayelipwa laki mbili anafanya kitu lakini wewe wa shilingi milioni na zaidi upo pale pale. Huna hata kiwanja, bado mpangaji.

Wako watu wa aina hiyo. Jiulize swali; wakati ulipata nafasi nzuri ya kazi, unaketi kiti cha kunesanesa, ulifanya nini? Kumbuka hicho kipindi kinapita.

Watu wengi wakishakuwa kwenye nafasi nzuri, maisha mazuri wanajua watakuwa hivyo daima. Wanasahau kuwa kipindi cha kuweka msingi ni cha muda mrefu. Ni kipindi cha maandalizi kwa hatua nyingine ya maisha.

Ni kweli kipindi kinapita, na kikishapita utaanza kukumbuka zile hela ulizokuwa unajaza kwenye mkoba, au kwenye droo ama za nyumbani au ofisini. Utaanza kuvuta droo kukumbuka lakini kiuhalisia hazipo tena kwani majira yalishapita.

Cha kujiuliza hapo ni je, ulipokuwa nazo ulizifanyia nini. Moja ya kitu ambacho adui atapigana nacho ni ile tunaita vita ya kujenga. Ni pale unapofanya au kupanga kitu chenye hatma yako ya kesho.

Kwa mfano unafanya kazi ukapata fedha, nunua basi hata kiwanja ambacho utakikuta kesho. Zaidi pia jenga nyumba ili uondokane na kodi. Mungu alikupatia muda mzuri kazini ili ujiwekee msingi wa kesho yako.

***Msomaji, niishie hapa.***

***Wiki ijayo nitaendeleza kwa mifano ya watu wanaojutia kutumia muda vibaya. Je, una maoni, kisa cha kimaisha? Tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Siasa iwekwe kando suala la machinga, mama lishe

WIKI iliyopita Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaa, Amos Makala, alitoa maelekezo ya kuwa na utaratibu maalum wa wafanyabiashara wadogo maarufu kama machinga na mama lishe ili kuhakikisha jiji limepangika.

Agizo hili limekuja kwa wakati mwafaka kwa kuwa jiji la Dar es Salaam na kwa mkoa kwa ujumla, linaonekana chafu na halina mpangilio kwamba mtu yeyote anaweza kufanya biashara kokote bila kuulizwa na yeyote na kutolipa kodi yoyote.

Kwa sasa njia za watembea kwa miguu hazipo. Ndiko wafanyabiashara hao wamejaa na mbaya zaidi walirudi hata katika maeneo wasiyotakiwa kama Posta na kubwa ni siasa kupewa nafasi kubwa kuliko uhalisia kwamba hawa ni wapigakura wasibugudhiwe.

Ukienda Kariakoo, idadi ya machinga imeongezeka kiasi kwamba hakuna pa kupita. Wamepanga bidhaa zao nje ya maduka, wateja wengi wadogo wanaishia kununua kwao huku wenye maduka ndio wanaolipa kodi.

Mwenge nako idadi inaongezeka kiasi kwamba kwa sasa hakuna sehemu za maegesho ya magari, huku maeneo ya watembea kwa miguu yaliyojengwa hivi karibuni kutokana na upanuzi wa barabara ya Mwenge - Morocco wameshajaa.

Ukienda Mbagala ndiyo kabisa wamejipanga hadi eneo la katikati ya hifadhi ya barabara na huku maeneo ya watembea kwa miguu yakimezwa yote.

Hali hii si ya kuridhisha kabisa kwa kuwa Dar es Salaam inakuwa na miavuli au mifuko ya nailoni mingi iliyosambazwa ili kupata kivuli huku usiku wakisambaza umeme ili kupata mwanga, jambo ambalo ni hatari sana.

Wafanyabiashara wenye maduka wanalipa kodi lakini wanashindwa kufanya biashara kiasi kwamba baadhi wamefunga maduka na kugeuza kuwa stoo za kuhifadhi mizigo ambayo husambazwa kwa wafanyabiashara wadogo na sasa ile kodi ambayo serikali ilikuwa inapata, haipati tena.

Ni muhimu sana kukawa na utaratibu kwa kuwapanga wafanyabiashara hawa kwa kuwa si kweli kuwa wanaruhusiwa kufanyabiashara zao kila mahali. Ni lazima kuwe na nidhamu ya ufanyaji biashara, na siyo kwamba wakifanya hivyo ndiyo wapigakura wazuri.

Haya yalifanyika kwenye mapito ya wanyama na maeneo ya mtawanyiko, ambayo yanapotea kwa kuwa vimesajiliwa vijiji, kufungiliwa mashamba na ofisi za serikali, kwa kisingizio cha wapigakura.

Hali hii iko katika miji yote na wakati utaratibu unafanyika ni muhimu kufungananisha sekta kama miundombinu mizuri na nishati, ili kuongeza mzunguko wa biashara kwenye miji midogo kwa ajili ya kupunguza wimbi la vijana wanaokimbilia mjini.

Mathalani, ukitembelea masoko ya Mabibo, Buguruni, Kariakoo na kwingine kuna idadi kubwa ya wavulana wanauza mifuko na kubeba mizigo baada ya muda hao ndiyo hugeuka kuwa machinga na kuanza kupanga bidhaa kando ya barabara.

Kwa sasa masoko mengi yana idadi kubwa ya wafanyabiashara walio nje ya masoko hayo. Mathalani, soko la Mabibo licha ya miundombinu duni lakini kwa sasa wafanyabiashara wanaanzia kwenye mchepuko wa barabara ya mwendokasi na wamefungua vibanda na kujaza mazao humo.

Kwa ujumla, serikali inapoteza mapato mengi kwa kuruhusu watu hawa kuongezeka na wako ambao hawakubali kuonyesha wamekuwa kibiashara kwa kuwa wanajua kinachofuata ni kulipa kodi.

Agizo la kuwapanga ni muhimu sana likatekelezwa hata kwa kujifunza nchi zingine ambazo zimefanikiwa kwamba waliweka kando siasa ya kwamba hawa wasibugudhiwe ni wapiga kura.

Ukitembelea jiji la Bangkok, Thailand, wametenga maeneo ya mama lishe ambao wako kwenye jengo kubwa katikati ya mji huku kwenye mitaa kuna eneo maalum na si kila mtu kujipangia bidhaa au kuanza kuuza chakula pale anakoona yeye kunafaa.

Pia kwa machinga wamepanga vizuri sana kiasi kwamba unaingia kwenye jengo kubwa lina machinga wa kila aina, na ndicho kinatakiwa kufanyika kwamba Kariakoo kuwe na maduka ya wauzaji wakubwa na machinga ambao wako kwenye eneo moja.

Hali ya sasa inaumiza nchi kwamba wale wanaotakiwa kufanya biashara ili walipe kodi wanashindwa na sasa kuna ujanja wa kufunga maduka na kubaki na stoo ya kuhifadhi mizigo inayosambazwa kwa machinga, hali ikiachwa hivi si sawa.

Dar es Salaam inapaswa kupangwa na ndiyo itakuwa mfano kwa miji na majiji mengine. Kuacha hali ilivyo ni kuharibu muonekano ambao siyo lazima mgeni atembelee bali akiwa angani anaona jinsi tulivyokosa mpangilio.

Machinga ni Watanzania wana haki ya kutafuta kipato lakini lazima kuangalia kasi ya vijana kukimbilia mjini, na kuhakikisha kuna kuwa na ukuaji sawa wa miji na majiji na kujenga mazingira wezeshi kwa vijana kubali vijijini kuzalisha na kupata mkate wa siku.

Wengi wanakimbilia mjini kwa kuwa ndiko kuna uwezekano wa kupata kipato, na bado shughuli za kilimo, uvuvi na ufugaji hazijajengewa mazingira wezeshi ya kuendelea kusalia waliko.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI














ILIKUWA shangwe na vigeregere wakati Maisala Juma na Said Ally Lwembe, walipofanya sherehe ya kujipongeza kudumu katika ndoa yao. Sherehe hiyo ilifanyika katika ukumbi wa Kivulini ulioko Mbagala Charambe jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

# MITINDO






MUSTAFA HASSANALI

## Mbunifu wa mavazi anayetamani kuona Tanzania inakuwa kinara



UKOSEFU wa sera, ubinafsi na kutopendana ni baadhi ya sababu zinazofanya tasnia ya mavazi kushindwa kusonga mbele kwa haraka.

Hayo yamesemwa na mbunifu maarufu wa mavazi nchini, Mustafa Hassanali, katika mahojiano maalum yaliyofanywa na gazeti hili. Hassanali ambaye anandaa jukwaa la maonyesho la Kimataifa la Swahili Fashion, alisema fani ya mavazi inashindwa kukua kwa haraka kama iliyo kwa mataifa mengine, kutokana na kutokuwapo sera inayowatambua na wadau kushindwa kufanya kazi kama ndugu.

Anasema imefikia wakati serikali kupitia Wizara ya Habari, Michezo, Utamaduni na Sanaa, inatakiwa kuwa na sera inayowatambua pamoja na kuwawekea mazingira rafiki ya kufanya kazi.

Mbunifu huyo, anasema kama kutakuwa na sera inayozungumzia umuhimu wa ubunifu na mitindo, ingetoa urahisi wa upatikanaji wa malighafi zinazotengenezwa na viwanda vya hapa nchini kuuzwa ndani.

Anasema, wabunifu wa mitindo pamoja na wadau katika fani ya mavazi, wanamuomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuliangalia suala hilo kwa umakini ili ifikie siku moja Tanzania inakuwa kinara wa kubuni mavazi katika Afrika na kujiingizia kipato.

“Kama mazingira yatawekwa sawa, naamini Tanzania siku moja itakuwa kinara katika sekta ya mavazi na kuiingizia nchi kipato kikubwa,” anaongeza kusema.

### UBINAFSI, KUTOPENDANA

Aidha, amesema tatizo la ubinafsi na kutopendana miongoni mwa wabunifu ni sugu linalowarudisha nyuma siku hadi siku.

Anasema inafikia wakati baadhi ya watu wanafanya hila katika kazi, ili kuhakikisha mwenzake asipate.

“Tatizo la ubinafsi na kuchukiana ni jambo baya sana, sasa inafikia watu kutibua mikataba ya kazi ili mwenzake akose. Nawaomba sana tuache tabia hii,” anasisitiza.

Anasema kama kungekuwa na ushirikiano, kazi zinapopatikana zingefanyika kwa ushirikiano kulingana na uwezo wa mtu na kuondoa dhana ya kukomoana.

### HATMA YA MAVAZI

Akizungumzia hatma ya fani ya mavazi nchini, Hassanali alisema mwenendo wake sio mbaya licha ya vikwazo mbalimbali vinavyojitokeza kila siku.

Anaamini siku moja fani hiyo itakuwa moja ya uwanja mpana wa ajira kwa vijana baada ya kuanzishwa viwanda vingi vya ushonaji na ubunifu wa mavazi.

UREMBO





EPUKA NGOZI KAVU

# Asali inatosha kulainisha, kukung'arisha

KATIKA kipindi hiki cha baridi na upepo wa kipupwe, watu wengi wanapata shida kutunza ngozi yao kutokana na kuwa kavu.

Mara nyingi baadhi ya watu wanaothamini urembo, wanatumia gharama kubwa kununua mafuta na vipodozi mbalimbali ili kuhakikisha ngozi inakuwa laini.

Hata hivyo, asali ni chakula kizuri, lakini inaweza kutumiwa kama kilainishi kizuri kuzuia ngozi kukauka au kupauka.

**HATUA YA KUCHUKUA**

Kama unataka kulainisha ngozi ya uso, unatakiwa kuchukua asali mbichi kijiko kimoja, paka usoni.



Baada ya kupaka kaa kwa dakika 15 hadi 20, halafu safisha uso wako kwa maji safi.

Hatua hii utafanya ngozi kujitibu na kuzuia kuota kwa chunusi.

Kama unataka kutoa uchafu kwenye ngozi, unatakiwa kuchanganya asali mbichi kijiko kimoja cha chakula na mafuta ya nazi vijiko viwili.

Mchanganyiko huo unapakwa usoni, kisha unatakiwa kujisugua taratibu kwa kufanya kama viduara huku ukiepuka kufikisha machoni. ukimaliza osha uso wako.

Unashauriwa kufanya hivyo mara kwa mara ili kupata matokeo mazuri kwa haraka. Kumbuka asali haina athari katika mwili na badala yake ni ina virutubisho vingi vinavyoleta faida mwilini.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Vyakula vya kupunguza unene

LEO nakupa mbinu ya kupunguza unene kwa kutumia vyakula. Haya ni baadhi ya mapishi ambayo yanasaidia kuondoa tatizo hilo kwa walaji.

**SUPU YA MAHARAGWE**

Maharagwe yana protini, nyuzinyuzi na hayana mafuta. Ni chakula kinachoshibisha haraka



na kwa muda mrefu bila kusababisha uzito kuongezeka.

**UAANDAJI**

Chukua viwango sawa vya ma-



haragwe, njugu mawe na mbaazi na chemsha kwa masaa kadhaa mpaka uone maharagwe na mbaazi zimetengana.

Weka karoti moja nzima ili inyonye gesi wakati wa kuchemsha.

Hapa unaweza kutumia supu hiyo uliyochemshia na kunywa baada ya kuongeza chumvi. Pia unaweza kuchuja maji na kuweka hayo maharagwe na vinginevyo katika supu ya nyama uliyoandaa pembeni na kuinywa.

**SUPU YA KABEJI**

Supu hii inasifika kwa kuwa na mbogamboga nyingi zinazopunguza uzito. Unavyoinywa zaidi ndivyo unavyopungua zaidi.

**UANDAAJI**

Kabeji moja kubwa ikatekate vizuri na vipande visiwe vidogodogo sana. Kitunguu maji kimoja kikubwa, kikatekate kama kawaida. Pilipili hoho moja kubwa ikatekate vizuri, kitunguu swaumu kifundo kimoja.

Chukua nyanya nusu kilo na katakata vipande vikubwa.

Karoti nusu kilo zikatekate saizi kubwa za kutafuna na maji lita tano. Kama una chombo kidogo, basi tumia maji lita mbili na nusu halafu gawanya kila kilichopo hapo juu kwa mbili.

Weka chumvi na pilipili kiasi, kaanga mbogamboga na vitunguu kwenye mafuta (mafuta ya nazi ni mazuri zaidi) kidogo (usiweke kabeji na nyanya).

Hakikisha vitunguu vinaiva lakini havibadiliki rangi kabisa. Ongeza nyanya, kabeji na maji na chemsha mpaka mbogamboga zilainike.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Hivi ndivyo unapaswa kuandaa chumba cha mtoto

PAMOJA na mambo mengine muhimu yanayohitajika katika kumjenga mtoto, ni chumba chake cha kulala. Anapofikia katika hatua fulani hususani ya kutambua kibaya na kizuri, ni kipindi mwafaka pia kwa ajili ya kumwandalia vitu vyake muhimu.

Ni vyema kutambua kuwa chumba hiki ndicho mtoto hutumia kufanyia shughuli zake nyingine ikiwamo kusoma na kucheza.

Mtoto ni baraka lakini ujio wake unahitaji pia maandalizi. Pamoja na hayo, ni vyema akawa na chumba chake ili pia kumjengea hali ya kujitegemea akiwa angali mdogo na pia kurahisisha uhifadhi wa vitu vyake bila kuchanganyika na vya wengine.

Chumba cha mtoto kinatakiwa kiwe ambacho atajisikia huru na kuhakikisha vitu vinavyowekwa ndani kwake vinavutia na vya kumfurahisha yeye.

Kitu cha kwanza kabisa katika kutengeneza chumba cha mtoto ni 'kudesign' mpangilio na kuhakikisha rangi zilizoko kwenye chumba hicho ni zile zenye utulivu na hakipaswi kufanana na cha watu wazima. Kinatakiwa kuwekwa vionjo hasa michoro ya kitoto kwenye kuta.

Weka midoli na michoro iliyo kwenye vibao vinavyohamishika au fremu za kuning'iniza.

Hakikisha samani zinazowekwa kwenye chumba hicho ni zile ambazo hazihatarishi usalama wake. Kwa mfano unaponunua kitanda cha mtoto, unanunua kile kinachozuia hata anapojigeuza. Anapokuwa amelala asianguke

Shuka, mito navyo vinatakiwa viwe rafiki kwa mtoto hasa kwenye rangi. Usichukue zile zinazotumiwa na watu wazima ukaweka kwenye chumba cha mtoto.

Kabati ya nguo na meza yake ya kusomea, navyo vinapaswa vitengenezwe kulingana na kimo cha mtoto ili iwe rahisi kwake kufikia vitu vilivyomo ndani yake.

Nunua samani ambazo zinaendana na mapambo yaliyomo katika chumba cha mtoto kulingana na jinsi yake kama ni wa kike hakikisha rangi zinakuwa za kike na kama ni wa kiume vivyo hivyo.

Mfano chumba cha mtoto wa kike hupendelea kuwa na rangi ya pinki. Ni vizuri mapambo na vitu vingine vilivyomo katika chumba chake vishabihiane na rangi hiyo ili kuleta muonekano mzuri na wa kumfurahisha.

Epuka kujaza samani kwenye chumba hicho cha mtoto kwa ajili ya usalama wake.

Baada ya hayo yote, weka vitu (toys) bora vya kuchezea mtoto wako.





## Dondoo muhimu namna ya kuchagua milango ya mbele




**1:** Hakikisha unachagua mlango wa mbele kwa umakini hasa kwa kuzingatia unakuwa na mbao ngumu na ujazo mkubwa.

**2:** Mlango unatakiwa kuwa na vipaa vya chuma vigumu kama komeo za ndani, kitasa na bawaba zenye viwango.

**3:** Mwonekano wa mlango uwe wa kuvutia, inatakiwa kuweka polishi au rangi ya mbao ambayo si ya kung'aa sana.

**4:** Flemu ya mlango wa mbele iwe ya milango miwili ili kumpa mtumiaji urahisi wa kuingiza vitu ndani.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2021
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
VIPI KAKA, MBONA SURA HAINA NURU KAMA UNASOTA KWENYE FOLENI YA SINDANO!
ACHA NKAZE ROHO NKILEWA NTAPATA JIBU
'MTENGULIWA'
KWA NINI UNAGONGA DAWATI UNAPOPATIA SWALI MPAKA UNAMUUDHI MWALIMU?
ANGEKUWA SPIKA WA BUNGE ANGEKUWA NA KAZI YA KUPITA KWA KILA MZAZI WA MBUNGE!
KERO YETU SISI NI KERO ZINAZOTUKERA KIASI KWAMBA IMEKUWA 'KERO!'
KAZI!!!
'NIYUU' DC'z
MINENO YENU INAWAUDHI WAKANDARASI KAMA HAMJUI... SISI MADEREVA FOLENI NI KAWAIDA
KAWAIDA WAPI! MBONA HAMPELEKI HESABU KAMILI KWA MATAJIRI? AU MNADHANI HATUJUI?
JAMANI UJENZI GANI WA BARABARA USIO NA FOLENI?
NTAMBABUA MTU VIBAO!...TUNAKAA MASAA KIBAO TUNACHELEWA MNA....!!!
UNA KIDETI KIPYA?
KWA NINI UNANIPANGIA KWA KUNILIPA PESA YANGU?
SIKUPANGII BALI UTARATIBU TU.... ULINIKOPESHA BAR NIKAKULIPIE BAR ISITOSHE KUNA 'PROMOSHENI'
NAKWENDA UKWENI LAKINI ROHO KAMA NAENDA 'JEHANAM!'
NDUGU HATUONANI KAMA UMEME UMEZIMIKA GHAFLA!
TUTAONANA NIKIZIKAMATA NAJUA SIMU HII UNACHOKONOA 'OFA'
HAPA MCHAWI 'DIKLOPA' SIO KUZODOA
INGLISHI TUPU!
VIPI USHAMPA MAKAVU YAKE?
NIMPE MAKAVU NAMPENDA...? NIMEYALOWEKA KWANZA
...KINYUNYIZO CHA LEO...
...PIPA LA POMBE HALILEWI

## Rais Nyusi aapa kuwatokomeza mbali wanamgambo Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, ameapa kuwamaliza wanamgambo wanaofungamana na kundi la kigaidi linalojiita dola la kiislamu kaskazini mwa nchi yake.

Rais Nyusi, alisema kazi ya kuwamaliza wanamgambo hao itafanywa kwa msaada wa washirika wake wa kikanda wanaojiandaa kupeleka jeshi la pamoja la ardhini. Jumuiya ya maendeleo ya nchi za kusini mwa Afrika (SADC) Jumatano ya wiki hii, iliidhinisha hatua ya kupeleka wanajeshi kusaidia kupambana na uasi unaosababisha umwagikaji wa damu katika mkoa wa Cabo Delgado tangu mwaka 2017.

Jumuiya hiyo haikuweka wazi ni kikosi cha wanajeshi wangapi kitakachopelekwa nchini humo, lakini Rais Nyusi jana katika hotuba yake ya maadhimisho ya miaka 46 ya uhuru wa nchi yake kutoka kwa Wareno , alisema wanamgambo wataangamizwa kwa msaada kutoka nje. Ureno na Marekani zinatoa mafunzo kwa wanajeshi wa Msumbiji, lakini ni mara ya kwanza kwa kiongozi huyo kuridhia msaada wa kijeshi kutoka nje kwa ajili ya kupambana na wanamgambo hao.

**DW.**

## UN yataka mazungumzo Syria

**NEWYORK,** MAREKANI

MJUMBE maalum wa Umoja wa Mataifa katika mgogoro wa Syria, Geir Pederson, ametowa wito wa kufanyika mazungumzo mapya ya kimataifa kuhusu kuchukua hatua za kuleta suluhisho la kisiasa.

Pederson, alitoa mfano wa hatua za kuchukuliwa ikiwa ni pamoja na kubadilishana wafungwa na usitishaji wa mapigano nchi nzima ambazo serikali na upinzani wanaweza kukubaliana kama juhudi za mwanzo.

Wito huo unatolewa wakati kukiwa hakuna hatua iliyopigwa kuelekea kuumaliza mgogoro wa miaka 10 nchini humo.

Pederson aliliambia Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kwamba anaamini maeneo aliyoyagusia na mengine,ndiyo yenye umuhimu zaidi kwa raia wa kawaida wa Syria na yana uwezekano wa kuleta msimamo wa pamoja miongoni mwa pande zinazozozana.

**DW**



Mfanyakazi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP), akiwa katika kijiji ambacho kimeathiriwa na baa la njaa kusini mwa Madagascar hivi karibuni. **PHOTO:WFP.**

# Baa la njaa lazidi kuitesa Madagascar

**ANTANANARIVO,** MADAGASCAR

SHIRIKA la mpango wa chakula duniani (WFP) limeonya baa la njaa linazidi Kusini mwa Madagascar na kutishia maisha ya maelfu ya watu ambao wako hatarini kuangamia kwa kukosa chakula.

Shirika hilo la Umoja wa Mataifa, lilieleza kwamba eneo hilo linakabiliwa na ukame kwa mara nyingine na kutishia kuwatumbukiza watu 400,000 kwenye njaa.

Tayari vifo vimeshuhudiwa kutokana na ukosefu wa chakula.

Mkurugenzi wa (WFP) kanda ya Kusini mwa Afrika, Lola Castro, aliwaambia waandishi habari siku ya ijumaa kwamba ameshuhudia hali mbaya ya watu wanaohitaji chakula alipoitembelea nchi hiyo hivi karibuni akiwa pamoja na mkuu wa shirika hilo David Beasley.

Madagascar ni kisiwa ilichoko kwenye ukanda wa bahari ya hindi, kikiwa na watu milioni 26.

Castro alisema alishuhudia mamia ya watu wazima na watoto wakiwa katika hali mbaya na wengine wakionekana wanyonge waliokondeana na walikuwa wakipewa msaada wa lishe.

Mkurugenzi huyo anayefanya kazi kwenye shirika hilo kwa miaka 28 sasa, alisema hajawahi kuona hali kama hiyo maishani mwake, ukiachana na ile hali aliyoishuhudia mwaka 1998, katika eneo la Bahr al-Gazal huko Sudan Kusini.

Umoja wa Mataifa na serikali ya Madagascar siku chache zijazo wataanzisha mwito wa kuchangisha fedha kiasi dola milioni 155 zitakazosaidia kununua chakula na kuyanusuru maisha ya watu.

Maelfu ya watu wameyakimbia makaazi yao kwenye maeneo ya vijijini na kukimbilia mijiji kwa lengo la kutafuta chakula, kwa mujibu wa mkurugenzi huyo.

Siku ya Ijumaa Beasley aliandika kwenye mtandao wa kijamii wa Twitter akieleza watu 400,000 wanaelekea kukosa chakula, huku 14,000 hawana kabisa chakula na ikiwa hatua za haraka hazitochukuliwa, idadi ya watu watakaoathiriwa na njaa itafikia 500,000, katika kipindi cha miezi michache ijayo.

Kwa mujibu wa maelezo ya mkurugenzi huyo wa WFP, familia zinaishi kwa kula matunda pori, majani na nzige kwa miezi kadhaa sasa.

Amesisitiza kwa hali hiyo haisababishwi na vita au migogoro, bali inatokana na mabadiliko ya tabia nchi. Aidha alikumbusha kwamba eneo hilo halijawahi kuhusika kwa namna yoyote kusababisha mabadiliko hayo ya tabia nchi, lakini sasa watu wake ndio wanaoandamwa na athari.

Shirika hilo pia limebaini kwamba watu milioni 1.14 kusini mwa Madagascar hawana chakula cha kutosha.

Ikumbukwe kwamba nchi hiyo haina migogoro lakini bado wananchi wake wanakabiliwa na janga la kibinadamu.

**DW**

# Merkel aitaja Hungary kama tishio

**BERLIN,** UJERUMANI

KANSELA wa Ujerumani, Angela Merkel, amesema anaamini kuwa msimamo wa Hungary katika mwelekeo wa Umoja wa Ulaya (EU) katika siku za usoni inaibua changamoto.

Kiongozi huyo alisema tatizo hilo linaleta tofauti kubwa baina ya taifa hilo na nchi nyingine wanachama. Akizungumza na waandishi wa habari baada ya mkutano wa wakuu wa nchi wa Umoja wa Ulaya, alisema kuna tofauti pana ya mitazamo juu ya hatma ya Umoja huo na mfano wa wazi ni misimamo ya serikali ya Hungary. Merkel alitolea mfano wa mapendekezo ya kupunguza nguvu za Bunge la Umoja wa Ulaya yaliyotolewa na nchi hiyo kupitia mkakati unaoendelea hivi sasa wa kukusanya maoni ya kuzifanyia mageuzi taasisi za umoja huo.

Matamshi ya Merkel yanafuatia mjadala mkali wa usiku wa Alhamisi uliochochewa na sheria mpya ya Hungary inayowapiga marufuku vijana kupata taarifa zinazohusu masuala ya wapenzi wa jinsia moja ambayo imekosolewa vikali na karibu wanachama wote.

**DW**

SAFU

MAKALA

# KATIBA NI MUHIMU KULIKO UTASHI WA MTU



Na Magabilo Masambu

**Ibara ya 107 B inasema" "Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi."**

DUNIANI kote sheria zozote zile haziko kama mapambo ya urembo harusini. Kazi kubwa ya sheria mahali popote, ziwe za nchi ama za kimila au za mahali fulani, zipo kwa ajili ya kudhibiti mwenendo na hulka za binadamu.

Kwa vyovyote vile, sheria hizo lazima ziwe na uwezo wa kuwadhibiti wanaosimamiwa pamoja na wale wanaozisimamia. Kosa kubwa ambalo tumekuwa tukilifanya ni kudhani kwamba wanaosimamia sheria hawapaswi kudhibitiwa na sheria hizo na kwamba wao wako juu ya sheria, hivyo kuwatoa kwenye kundi la ubinadamu kama walivyo wengine.

Tanzania tunayo Katiba ya Nchi ya mwaka 1977. Katiba hii kwa jinsi ilivyo sasa na mamlaka iliyompatia Rais, ni wazi kwamba inamfanya yeye mwenyewe asiitumie na badala yake kuongoza nchi kwa kutumia utashi wake, bila kuitumia kama sheria mama ya sheria zingine zote.

Miaka yote tumekuwa tukiamini kwamba mihimili ile mitatu kwa maana ya Serikali, Mahakama na Bunge kila mmoja uko huru kumbe si kweli, bali miwili kwa mujibu wa Katiba ya sasa haiko huru katika utendaji wake wa shughuli za kila siku na ushahidi wake ni huu.

Ibara ya 107 B inasema" "Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, mahakama zote zitakuwa huru na zitalazimika kuzingatia tu masharti ya Katiba na yale ya sheria za nchi."

Lakini ukisoma Ibara ya 118(2) inasema: "Jaji Mkuu atateuliwa na Rais na atakuwa ndiye Kiongozi wa Mahakama ya Rufani na pia Mkuu wa Idara ya Mahakama kama ilivyofafanuliwa katika ibara ya 116 ya Katiba hii."

Si Jaji Mkuu tu anayeteuliwa na Rais bali hata majaji wengine wa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu wateteuliwa na Rais, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kutoka miongoni mwa watu ambao wanaweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama Kuu ya Jamhuri ya Muungano kama ilivyoelezwa katika ibara ya 109 ya Katiba hii na hii ni kwa mujibu wa ibara ya 118(3)

Kwa upande wa Bunge, mtendaji mkuu wa ofisi ya Bunge huteuliwa na Rais na hii ni kwa mujibu wa ibara 87(1). Ibara hiyo inasema: "Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano."

Katibu wa Bunge ni nani? Ibara ya 87(2) inafafanua: "Katibu wa Bunge atakuwa ndiye mtendaji mkuu katika Ofisi ya Bunge na atawajibika kwa utendaji bora wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii na ya sheria inayohusika"

Ibara ya 37(1) inasema: "Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii, na sheria za Jamhuri ya Muungano katika utendaji wa kazi na shughuli zake, Rais atakuwa huru na hatalazimika kufuata ushauri atakaopewa na mtu yeyote, isipokuwa tu pale anapotakiwa na Katiba hii au na sheria nyingine yoyote kufanya jambo lolote kulingana na ushauri anaopewa na mtu au mamlaka."

Funga kazi ni ibara ya 46(1), (2) na (3). Ibara hii inapiga marufuku kwa namna yoyote ile kumfungulia mashitaka Rais ama akiwa madarakani au akiwa ametoka kuhusu makosa yoyote aliyoyatenda ama kabla ya kuwa Rais au akiwa na madaraka ya urais.

Huo ni baadhi ya upungufu nilioouona katika Katiba yetu unaoweza kumfanya Rais akaendesha nchi kwa kutumia utashi wake kuliko kudhibitiwa na Katiba. Huwezi kuwa na mahakama huru ambayo inaongozwa na mtu aliyeteuliwa na Rais. Kwa maana nyingine, ajira ya Jaji Mkuu ambaye kisheria ndiye mtendaji mkuu wa mahakama iko mikononi mwa Rais.

Huwezi kuwa vilevile na Bunge huru kama mtendaji mkuu wa bunge naye anateuliwa na Rais, halafu ukawa na Katiba inayosema katika utendaji wake Rais hatalazimika kufuata ushauri wa mtu yeyote na pia mwenye kinga ya kutoshitakiwa. Ina maana Rais ana uwezo wa kukataa hata ushauri wa Jaji Mkuu au Mwanasheria Mkuu wa Serikali au wa Spika wa Bunge.

Kuna umuhimu mkubwa sana wa kukubaliana kama nchi kwa pamoja kufanya mabadiliko ya Katiba kwa sababu yeyote anaweza kuwa Rais katika nchi hii. Bahati mbaya tu ni kwamba wenye madaraka wanafikiri kwamba hitaji la mabadiliko ya Katiba ni la wale wasiyo na madaraka, lakini wanapoyakosa madaraka ndiyo huona umuhimu wa mabadiliko hayo kwa sababu na wao huathirika na mabadiliko ya uongozi.

Tunapaswa kuwa na Katiba ambayo itamfanya yeyote kuwa Rais na asilete tabu katika nchi kwa kutumia utashi wake, bali adhibitiwe na Katiba. Mfano, tutakapokuwa na Katiba itakayoruhusu Rais kushtakiwa, maana yake wakati wa uongozi wake atakuwa na tahadhari kubwa kuepuka kuchukuliwa hatua za kisheria

Kwa Katiba ya sasa kama haitafanyiwa marekebisho, kuna siku tunaweza kumpata Rais atakayetuamrisha wote nchi nzima tutale saa 8:00 mchana kwamba ni usiku kwa sababu Rais wa Tanzania anatolewa kwenye kundi la ubinadamu na kwamba yeye sasa ni malaika hatendi makosa.

Katiba imetufanya wananchi kutoziamini tena taasisi zingine, badala yake kila jambo likifanyika mathalani, mishahara ikiongezwa, mahakama ikiwaachia watu huru, waliodhulumiwa wakirudishiwa fedha zao, utasikia tunamshukuru Rais.

Si jambo baya kumshukuru Rais lakini hii shukuru ya sasa ni ushahidi kwamba tunaamini yote yanayofanyika katika nchi yana mkono wa Rais, yawe mema au mabaya. Katiba bora itaweka misingi ya mihimili yote kuonekana inafanya kazi ikiwa huru na itaaminiwa.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Visa vya kina Mzee Jongo, Jangala*



Na Adam Fungamwango

**Kuna mchezo mmoja wa jamaa ambaye alimtelekeza mkewe na kwenda kuishi kwa kimada, lakini baada ya pesa kumalizika alirudi kumwomba radhi mkewe. Mzee Jongo ni mmoja wa wazee walioitwa ili kumaliza tatizo hilo.**

HAKUKUWA na televisheni wakati huo Tanzania Bara. Televisheni Bongo zilianza kuingia mwanzoni mwa miaka ya 1990 tena kwa watu wachache tu. Zilianza kutapakaa sasa angalau unaweza kukuta baada ya nyumba 10, mmoja anayo.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990 hata zilipoingia hakukuwa na vituo vya televisheni. Labda Zanzibar tu. Na hata kupatikana kwenyewe ilikuwa shida. Wengi TV walizitumia kwa kuangalia mikanda ya video. Ndio wakati ilipoingia mikanda mingi ya picha za kizungu, kihindi pamoja na muziki kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) hasa ya kina Aurlus Mabele, Kanda Bongoman, Pepe Kalle na Soukous Stars.

Mada hii ni pana na ipo siku nitaizungumzia kwa urefu, jinsi ujio wa televisheni nchini ulivyotangaza sana miziki ya Kikongo nchini Tanzania.

Wakati nchi ikiwa bila TV, kitu pekee kilichokuwa kikiwahabarisha Wabongo ni redio, tena nazo huwezi kukuta kila mtu anayo. Vijijini inawezekana anayo Mwenyekiti wa Kijiji tu na ilikuwa vipindi maalum na wakati husika wa kwenda kusikiliza.

Walimu na watu waliokuwa wakifanya kazi serikalini au bomani, ndio walioonekana kumudu kuwa nazo. Si mikoani tu, hata Dar es Salaam. Unaweza kutembelea nyumba 10 ukakuta moja tu ndiyo yenye redio.

Zilipoingia televisheni, nchi ilipata mastaa wa tamthilia na filamu kama kina Steven Kanumba, Vincent 'Ray' Kigosi, Wema Sepetu, Irene Uwoya na wengine wengi. Hawa walikuwa wanaonekana kwa macho, baada ya kuingia kwa televisheni. Kabla ya hapo kulikuwa na mastaa wa michezo ya kuigiza.

Hawa hawakuwa wanaonekana kwa macho. Walikuwa wanasikika tu kwenye redio. Lakini michezo yao ilikuwa maarufu sana wakati huo na wao kuwa maarufu. Kwa bahati mbaya hata wakionekana kwenye macho ya watu hawajulikani. Labda mpaka uambiwe huyu ndiye fulani. Hawa ndio mastaa wa zamani.

Mmoja wa waigizaji waliokuwa maarufu wakati huo ni Ibrahim Raha ambaye alijulikana kwenye michezo ya kuigiza kama Mzee Jongo. Mwingine ni Bakari Mbelemba, maarufu kama Mzee Jangala. Ni waigizaji waliojichukulia umaarufu mkubwa wakati huo kutokana na aina yao ya uigizaji.

Mzee Jongo ambaye ni marehemu, alikuwa mzee mwenye vituko, mtata, ambaye pia alikuwa na tabia ya kumweleza ukweli mtu hapo hapo, bila kuzungusha maneno au kusubiri wakati fulani. Lafudhi yake ya Kizaramo ilikuwa burudani tosha pamoja na kushindwa kutamka baadhi ya maneno ya Kiswahili kwa ufasaha.

Kuna mchezo mmoja wa jamaa ambaye alimtelekeza mkewe na kwenda kuishi kwa kimada, lakini baada ya pesa kumalizika alirudi kumwomba radhi mkewe. Mzee Jongo ni mmoja wa wazee walioitwa ili kumaliza tatizo hilo. Jamaa akawa anamwambia mkewe "mke wangu nipokee."

Mzee Jongo akamwambia "We mwombe vizuri mkeo ili akusamehe. Unamwambia akupokee, kwani umekuja na treni?" Hivi ni moja kati ya vituko vya mzee huyo.

Mchezo mwingine ni wa jamaa aliyekuwa mwizi. Alikwenda kuiba bandarini wakamkamata, wakampiga na kulazwa Muhimbili. Majirani walipoambiwa waliogopa kwenda kumpa habari mkewe.

Mzee Jongo kama kawaida yake akajitolea akaenda kumwambia: "Mumeo kenda homola bandarini. Basi wamemkamata. Wamembomoa kweli kweli. Ukimwona mumeo hivi sasa utamsahau. Mumeo kana songo. Migulu bogojo. Mizino fumu."

Hapa alikuwa anampa habari mke wa jama huyo mwizi kwa kiswahili kilichochanganyika na Kizaramo. Alikuwa anamwambia mumewe ameenda kuiba bandarini, wamemkamata na kumpiga. Mumewe sasa ana chongo. Miguu imevunjwa na baadhi ya meno yametoka.

Ilifika wakati mchezo wa kuigiza wowote wa Redio Tanzania Dar es Salaam (RTD) bila Mzee Jongo kwa mashabiki ilionekana kama haujakamilika.

Mwingine ni Mzee Jangala. Huyu bado yupo. Tabia zake hazitofautiani sana na Mzee Jongo. Ni mtata. Yeye lafudhi yake ni ya watu ya Rufiji mkoani Pwani na kidogo kama Ifakara mkoani Morogoro. Ni mzee mtata, mbishi mwenye msimamo mkali. Alikuwa na uwezo wa kusimamia anachokiamini hata kama atakuwa peke yake wakati wote waliobaki wako upande mwingine.

Moja ya mchezo wake au igizo lake kwenye redio liliitwa 'Niachieni Mwenyewe.' Alikuwa na kijana wake Mshamu ambaye alimdekeza kupita kiasi. Lakini baadaye matokeo yake aliyaona.

Kingine ni kwamba Mzee Jangala hata kama atasimamia jambo ambalo liko kinyume cha jamii na watu wote hawakubaliani nalo, bado ana uwezo mkubwa wa kujenga hoja nzito kulihalalisha, kiasi kwamba hata baadhi ya wanaosikiliza wanaweza kuamini kuwa yuko sahihi. Hii ndiyo maana halisi ya mwigizaji au msanii.

Wasanii hawa wawili walisababisha watoto, vijana na kinamama siku ya mchezo kufanya kazi zao mapema na kukaa kusubiri muda wa mchezo wa kuigiza.

Walisaidiana na baadhi ya wasanii kama Janja, Zena Dillip, maarufu kama Siwema Binti Mtayaona, ambaye uigizaji wake hautofautiani sana na Bi Hindu. Wengine ni Hamisi Tajiri, Ally Keto, Mzee Igunanilo na wengineo.

# HADITHI

KWANI mapenzi ni nini? Si kumpenda yule unayemtaka wewe? Kwa nini inafika wakati watu wanapangiana? Je, ukilazimisha yanaitwa mapenzi? Si yatafanana na utumwa? Yeyote anayetaka kulifanya penzi liwe na matabaka, rangi, kabila, anaweza kusababisha maafa makubwa. Donald. Kijana msomi aliyetoka Marekani, anarejea nchini Tanzania. Anakabidhiwa kuendesha kampuni za baba yake. Lakini pia anatakiwa aoe. Hapo ndipo tatizo linapoanza. Usikose hata nakala moja ya riwaya hii tamu na ya kusisimua.

# Sumu ya mapenzi-12

**Na Adam Fungamwangwo (0716 350534)**




Pesa iongezwe mzee."

"Wee, nisikilize kwanza, pesa haina tatizo. Ni kwamba awali huyo kijana hakuwa kwenye mipango, lakini naona anaweza kuwa hatari kwako na kwangu kama tukimuacha."

Peterson na Bogota walikuwa wakiongea maneno hayo kwenye simu kwa tahadhari, wakikwepa kutamka maneno halisi kwa kuhofia sauti zao kunaswana mamlaka husika na kuweza kufuatiliwa.

Mpango wa kuondoa uhai wa dereva wa bodaboda aliusuka mwenyewe mzee Peterson kwa kuhofia siri kuvuja. Alihofia kumhusisha mkwewe mtarajiwa Doroth kwa sababu ni mtu wake anayemuamini, hivyo alijua hatoweza kukubali na huenda mpango huo ukavurugika.

"Cha kufanya ni kumalizana kwanza na huyo dada, halafu huyo bodaboda kwanza muache. Atakapotoka hapo mfuatilie na kwenda kumalizana naye sehemu nyingine kabisa, sawa Bogota?"

"Mimi pia si nina pikipiki? Nitakula naye sahani moja."

Baada ya kukata, kwenye simu yake hiyo aliangalia saa. Ilimuonyesha kuwa ilitimia tatu kasorobo.

Aliitengeneza bastola yake vizuri kwa ajili ya kuifanya kazi aliyotumwa.

Zilipita zaidi ya bodaboda kumi. Asilimia 90 abiria wake walikua ni wa kike. Lakini si aliyemhitaji.

Wakati akitaka kujisahau, alisikia sauti ya bodaboda nyingine. Ilikuwa mbali kidogo, lakini alipigwa na mwanga mkali wa taa.

Ilipofika karibu alijitahidi kukaza macho. Alichokiaona ndicho alichoambiwa. Abiria aliyekuwa nyuma ni yule aliyeambiwa na mzee Peterson.

Ghafla alijikuta akitoa bastola yake kutaka kuitumia.

Alisita. Si kwa sababu alikuwa na huruma. Bogota hakuwahi kuwa na huruma hata mara moja. kazi yake hiyo haikumtaka kuwa hivyo.

Ni kwamba kasi ya bodaboda ilikuwa kubwa mno. Aliona akipiga risasi anaweza kumkosa na mipango ikavurugika. Ni kwa sababu sauti ingekuwa imewashtua watu wengi, lakini mlengwa akiwa bado yu hai.

Awali alidhani itakuwa rahisi tu akipita na kumuona, atatoa bastola na kufanikisha mpango wake.

**Ghafla alijikuta akitoa bastola yake kutaka kuitumia. Alisita. Si kwa sababu alikuwa na huruma. Bogota hakuwahi kuwa na huruma hata mara moja. kazi yake hiyo haikumtaka kuwa hivyo.**

Alilazimika kubadili mbinu. Alipanda pikipiki yake na kuifuata. Mikononi akiwa na glovu. Alivaa kofia nyeusi kwa ajili ya kuzuia sura yake kuonekana. Hakuna yeyote aliyehisi chochote ambacho si cha kawaida.

Wakati anakaribia kuwafikia, aliwaza jinsi atakavyomaliza kazi. Hakutaka windo la pili kudhurika. Alikumbuka maneno ya bosi wake mzee Peterson kuwa dereva alitakiwa ashughulikiwe mbali na hapo.

Kitendo cha kumchapa risasi msichana, kingemfanya dereva naye kuanguka na bodaboda kwa hofu, akaumia, au kujeruhiwa vibaya, kitu ambacho hakikupangwa.

Kwa uzoefu wa mambo hayo ndiyo maana alibadili mpango. Alipofika karibu alizidisha mwendo na kuigonga kwa makusudi kwa nyuma. Ikayumba. Kwa ustadi alimsukuma Tausi na mkono wake wa kushoto, ambaye tayari alikuwa ameingiwa na hofu kwa kilichotokea. Kutokana na spidi ya bodaboda alipaa na kwenda kuangukia kwenye mtaro.

Said alikuwa bado anajitahidi kuiweka vizuri bodaboda yake iliyokuwa ikiyumbayumba bila mpangilio.

"Umeua." Bogota alipaza sauti kumwambia dereva wa bodaboda. Lengo ilikuwa ni kumchanganya.

Said alijua ni kweli ameua. Akawa hajui asimame na bodaboda yake au akimbie.

"Tulia tulia kwanza. Simama." Bogota alimwambia. Akasimamisha. Alikosea. Hakujua lengo la Bogota. Ni jamaa mwenye akili kama mchwa. Kama angeitumia akili hiyo vizuri angekuwa mbali sana. Hakutaka Said aondoke muda huo kwani anamhitaji.

Lakini kwanza alitaka kukamilisha kazi ya kwanza. Hivyo angemuachia, Said angekuwa kilometa nyingi kabla hajamalizana na Tausi. "Ngoja kwanza nimuangalie, inawezekana kachubuka tu." Bogota alisema huku akirudi nyuma na kuangalia kwenye mtaro mrefu. Kwa mbali alimuona Tausi akijikunjakunja kuugulia maumivu. Ndipo alipojua kuwa bado yu hai, ingawa yuko kwenye maumivu makali.

Kitendo bila kuchelewa, alitoa bastola yake na kuachia risasi mbili zilizosababisha atulie kimya.

Milio la risasi ilimchanganya Said. Hakumuona Bogota alichofanya. Alidhani labda ni majambazi ambayo yamevamia kwenye moja ya baa zilizotapakaa Sinza "Kimbia." Sauti ya Bogota ilimuamuru.

Kama umeme. Said alipanda pikipiki yake na kuondoka kwa kasi. Alikuwa akirejea alikotoka.

Ndicho Bogota alichokuwa akikitaka. Naye alipanda pikipiki yake na kumfuata.

Alipofika Sinza Kijiweni alikata kona kushoto kuelekea njia ya kwenda Tandale.

Ni ile ile aliyojia.

Bogota pia aliifuata. Alikuwa akitafuta sehemu nzuri ambayo angetekeleza alichotumwa na mzee Peterson. Sehemu aliyokuwa akiihitaji ni daraja la Manzese Uzuri. Mita chache kabla ya kufika, akiwa amemkaribia kwa hatua kama 15 hivi, alipunguza mwendo akashika stelingi ya pikipiki upande mmoja, mwingine ukiwa na bastola, alilenga chini ya bodaboda ya Said na kuachia risasi moja.

Hiyo ilitosha kupasua gurudumu na vyuma kadhaa chini, ikiifanya bodaboda kukosa uelekeo na kuyumba. Ilikwenda kugonga kingo za daraja. Alisogea karibu na ajali ile. Alichofanya ni kuongeza risasi nyingine kwenye mwili ya Said ambao ulikuwa uko chini kando kingo hizo, bodaboda ikiwa pembeni yake. Kwa uzoefu wake alijua tayari amemaliza kazi. Aliondoka kwa kasi na pikipiki yake kuelekea maeneo ya Tandale Magharibi.

INAENDELEA JUMAPILI



# ROMY JONES KUJA KIVINGINE

MKALI wa kuchezeshga mashabiki, Romy Jones, amesema muziki umebadilika sasa watu wanataka muziki wenye staha na unaochezeka nje.

Amesema anatarajia kuanzisha kiwanja maalum cha watu kufurahia maisha kwa kuwachezesha watu sehemu ya wazi badala ya ukumbini kama ilivyokuwa zamani.

"Muziki umebadilika, watu wanataka mapiano na mwendo wa taratibu kama ilivyo sasa, nadhani nitaanzisha burudani ya nje ili kila mtu aburudike bila kutokwa jasho," amesema Jones.

# Tamasha la Injili kutikisa Nyarugusu

WAIMBAJI wa kundi la muziki wa Injili kutoka kambi ya wakimbizi ya Nyarugusu nchini, New Generation Gospel Band For Christ ( NGGBC), wanatarajia kufanya tamasha kubwa kwa ajili ya kumtukuza Mungu.

Mwandalizi wa tamasha hilo, Thomas Mwene, alisema tamasha hilo limeandaliwa mkoani Kigoma kuanzia Julai 4, kwenye kambi Nyarugusu ndani ya jengo la kanisa la CADAF. Amesema burudani hiyo itaanza saa saba mchana hadi 12 jioni.

**NGGBC NI NINI?**

Kundi hili lilianzishwa mwanzoni mwa mwaka 2014, likiwa na lengo la kufundisha vijana kumjua Mungu kupitia muziki.

NGGBC lilianza na vijana waliojiunga kutoka makanisa mbalimbali ambao walikuwa hawajaokoka na wengine wamerudi nyuma kiroho, kupitia kundi hilo sasa hivi wanazidi kuimarika. Kundi lilianzishwa na M'msa Makobola chini ya mbeba maono Yoheli Makeci Ebuela, maarufu kama Joel Makeci.

**CHANGAMOTO**

Kundi hili lililoanza kama bendi ya muziki wa Injili likiwa na matumaini ya kujitegemea kama taasisi zingine za kidini.

Hata hivyo, wakati linaimarika likapata changamoto ya viongozi wakuu kwenda nchi za Ulaya na Marekani mwaka 2017.



# Tundaman aiba pochi la mkewe

DUNIANI kuna vituko! Wiki hii mwanamuziki mkongwe wa Bongo Fleva, Tundaman, amejikuta akitembea na pochi la wanawake baada ya kuiba kwa ajili ya kuhifadhi simu zake.

Tundaman ametokelezea na pochi hiyo kwenye shoo ya Friday Night Live, inayorushwa na East Africa TV na East Africa Radio siku ya Ijumaa.

"Mke wangu ndio huwa anajua kwamba kabla sijatoka natakiwa nivae nini ili niwe sawa ananisimamia kwenye upande wa mavazi, nimetoka na hii pochi kwa sababu simu yangu kubwa na mfukoni haikai, nimekikuta sehemu yake anayoweka pochi nikakichukua kukivaa na hajui kama nimekichukua" amesema Tundaman.



# Tierney asaini miaka 5 Arsenal

**LONDON,** England

KIERAN Tierney amesaini dili la muda mrefu kuitumikia Klabu ya Arsenal inayonolewa na kocha Mkuu, Mikel Arteta.

Tierney amesema kuwa ilikuwa ni jambo la haraka kwake kuamua kukubali kubaki ndani ya kikosi cha Arsenal kwa kuwa anaona milango ya mafanikio kwake akiwa ndani ya Emirates.

Alijiunga na Arsenal msimu wa 2019 akitokea Klabu ya Celtic na amekuwa ni mchezaji muhimu mbele ya Arteta licha ya kwamba amekuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara wa mara, akiwa amecheza jumla ya mechi 62 na alitwaa taji la FA katika msimu wake wa kwanza.

Beki huyo wa kushoto amesema kuwa anaamini kwamba uwepo wake ndani ya Arsenal ni faida kwake kwa wakati huu na ujao hivyo hana mashaka ya kusaini dili la muda mrefu kwenye kikosi hicho.

Kwa upande wa Arteta amesema kuwa Tierney ni moja ya wachezaji muhimu kwake na anaamini watafanya vizuri jambo ambalo limemfanya ampe dili la muda mrefu.

"Ni mchezaji mzuri anastahili kupewa mkataba mrefu hivyo imani yangu ni kuona kwamba hapo baadaye atafanya kazi nzuri ndani ya Ligi Kuu England," alisema.







# CHELSEA YAJIPANGA KWA HAALAND

**LONDON,** England

CHELSEA inakusudia kufanya kila linalowezekana kupata saini ya Erling Haaland msimu huu wa joto, kwa mujibu wa Eurosport.

Vyanzo vya karibu na Chelsea vinasema vina matumaini kwamba klabu hiyo itajaribu kina cha maji kwa Borussia Dortmund iwapo inaweza kuruka foleni na kumsajili nyota huyo raia wa Norway mwaka mmoja kabla, klabu nyingi zikitarajia kuingia sokoni kwa ajili ya mshambuliaji huyo.

Dortmund haina mpango wa kumuuza Haaland msimu huu, bado hali hiyo haina maana uhamisho hauwezekani.

Na sasa Chelsea ina uwezekano mkubwa zaidi wa kufuatilia dili hilo.

Real Madrid ni moja ya klabu inayotajwa kuwa kwenye nia ya kutaka kumsajili Haaland.

# Mbappe ataka kuondoka PSG

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amewaambia mabosi wa klabu yake ya Paris Saint-Germain kwamba anataka kuondoka.

Hilo linasemwa wakati mkali huyo wa kimataifa wa chama la Les Bleus akihusishwa na miamba ya soka ya Hispania, Real Madrid.

Mbappe mwenye umri wa miaka 22, mkataba wake kwenye kikosi hicho cha PSG utafika tamati mwakani na haonekani kabisa kuwa na dalili ya kusaini dili jipya la kuendelea kukipiga kwenye timu hiyo inayonolewa na Mauricio Pochettino.

PSG iliweka wazi kwamba haitaki kumpoteza bure Mbappe, lakini bado haitaki kuchekelea ofa zinazoletwa kwenye timu hiyo kwa ajili ya kutaka saini ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia.

Lakini, kwa sasa Mbappe amewaambia miamba hiyo ya Ligue 1 anataka kuondoka, kwa mujibu wa RMC Sport - huku mchezaji mwenyewe akivutiwa na mpango wa kwenda kukipiga Santiago Bernabeu.

Mwandishi wa RMC Sport, Daniel Riolo alifichua: "Nafahamu kwamba Mbappe ameomba kuondoka.

"Lakini, habari ni kwamba hataki kubaki - kwa sababu mchezaji mwenyewe haamini mipango ya Leonardo."

"Kama hataondoka kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya kiangazi, atakuwa mchezaji huru msimu ujao - na huko Doha (kwa wamiliki wa PSG) hawataki kabisa kusikia hicho kitu.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SANCHO AKARIBIA KUSAINI MAN UTD

●●● Dortmund yakubali kitita kipya na atasaini mara baada ya...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United, wamekubali kutoa kitita cha pauni milioni 77 kwa ajili ya kupata saini ya nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho.

Inaelezwa kuwa United wanataka saini ya Sancho mwenye umri wa miaka 21 ikiwa ni usajili wao wa kwanza na tayari Dortmund imekubali kumuuza nyota huyo.

Habari zimeeleza kuwa awali Dortmund walikuwa wanahitaji pauni milioni 100 lakini sasa wameshusha mpaka pauni milioni 77.

**Awali Man United ilipeleka ofa kwa mabosi wake kumpata nyota huyo na ilikataliwa na sasa imeelezwa kuwa imejibu na kilichobaki ni kusaini mkataba wa miaka mitano na timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu England.**

Man United walikaribia kumsajili Sancho kuelekea msimu wa 2020-21, lakini dili hilo lilishindikana.

Lakini sasa miamba hao wa Ligi Kuu ya England, wamejiweka kwenye nafasi nzuri zaidi ya kumsajili kuelekea msimu wa 2021-22.

Mwandishi wa habari wa Sky Sport Italia, Fabrizio Romano amethibitisha kwamba, dili la Sancho kutua Man United limefanikiwa.

Romano amesema kwamba Sancho atasaini mkataba na Man United mara baada ya kumalizika kwa michuano ya Euro 2020 ambapo yeye yupo na kikosi cha England.

## ZISIKUPITE

### VARANE AITAKA MAN

MLINZI wa Real Madrid, Raphael Varane, 28, anataka kujiunga na Manchester United wakati huu wa majira ya joto, lakini huenda mchezaji huyo raia wa Ufaransa akakwamishwa na mshahara anaoutaka wa euro 400,000 kwa wiki. ***(Independent)***

### SPURS WAMTAKA GERRARD

KLABU ya Tottenham Hotspur wanamtaka kocha wa Rangers, Steven Gerrard, kama watashindwa kumpata kocha wa zamani wa Wolves, Nuno Espirito Santo. ***(Evening Standard)***

### COOPER ANUKIA PALACE

CRYSTAL Palace, huenda wakabisha hodi kwa kocha wa Swansea, Steve Cooper, baada ya kukwaa kisiki kwa kocha wa zamani wa Borussia Dortmund, Lucien Favre.

### MARTIAL KUUZWA

MANCHESTER United huenda wakakubali kitita cha fedha ili kumtoa mshambuliaji wao raia wa Ufaransa, Anthony Martial, 25, na kiungo Mholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24.***(Mail)***

### MESSI KUSAINI

LIONEL Messi ameanza mazungumzo na Barcelona kwa ajili ya kusaini mkataba mpya. Mkataba wake unamalizika mwisho wa mwezi huu. ***(Marca)***

### WERNER HAONDOKI CHELSEA

LICHA ya kuhusishwa na kuhamia Real Madrid, wakala wa mshambuliaji, Timo Werner rai wa Ujerumani amesisitiza kuwa atabakia Chelsea. ***(BT Sport)***

### SMALLING AWANIWA EVERTON

KLABU ya Everton inahusishwa na uhamisho wa mlinzi wa AS Roma ya Italia, Chris Smalling, 31. ***(Mail)***.

### KOUNDE ATAKIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur wanataka kuimarisha sehemu ya ulinzi kwa kumsajili mlinzi wa kati rai wa Ufaransa anayekipiga katika klabu ya Sevilla, Jules Kounde, 22. ***(Sky Sport)***

### BENITEZ ATAJWA EVERTON

EVERTON imeingia kwneye rada za kuwania kumchukua Rafael Benitez kuwa kocha wao mpya.***(BBC Sport)***

### DANCHEZ ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL imevutiwa na kiwango cha kiungo raia wa Ureno, Renato Sanches, ambaye ameonesha kiwango kikubwa wakati wa michuano ya mataifa ya Ulaya yanayoendelea akiichezea Ureno. ***(Mail)***

### ROWE AWANIWA ASTON VILLA

ASTON Villa inataka kuweka dau la pili ili kumnyakua kinda wa Arsenal raia wa England, anayecheza nafasi ya kiungo mshambuliaji, Emile Smith Rowe, 20. Dau la awali la euro milioni 25 lilikataliwa. ***(Sun)***

## HABARI MICHEZO

## ZFF kuchagua rais leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar, ZFF, Leo Jumapili linafanya uchaguzi wa Rais atakayeongoza kwa kipindi cha miaka minne.

Uchaguzi huo unafanyika baada ya kujiuzulu kwa liyekuwa rais wa shirikisho hilo, Seif Kombo Pandu mapema Februari mwaka huu.

Uchaguzi huo utafanyika katika ukumbi wa Chuo cha Mafunzo kilichopo Kilimani chini na unawashirikisha wajumbe 24 ambao ndio watakaopiga kura kutoka katika klabu pamoja na vyama vya ZFF.

Wajumbe hao ni 24 ikiwamo wajumbe 10 kutoka katika klabu 10 za ligi kuu ya Zanzibar.

Wajumbe wengine ni kutoka vyama vya soka kwa mikoa yote mitano ya Zanzibar.

Kwa upande wa vyama vingine ni Chama cha Madaktari wa Michezo mjumbe mmoja, Chama cha Makocha mjumbe mmoja, Chama cha Soka cha Watu Wenye ulemavu, mjumbe mmoja pamoja na Chama cha haki na hadhi za wachezaji mjumbe mmoja.

Jumla ya wagombea watano wamejitosa katika kinyang'angiro hicho ambao ni Abdulatif Ali Yassin, Suleiman Mahmoud, Jabil, Suleiman Shaban Suleiman, Abdulkadir Mohmed Abdulkadir "Tash" na Haji Shehe Hamad.

## Morocco: Mechi zilizobaki ni ngumu

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Hemed Morocco amsema mechi mbili zilizobakia za Ligi Kuu Tanzania Bara, zinampa wakati mgumu kuhakikisha anatafuta pointi 6, zitakazomuweka kwenye mazingira mazuri ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Namungo iko nafasi ya tano ikiwa na pointi 43 na imebakiza mechi hizo mbili dhidi ya Ruvu Shooting mchezo utakaopigwa Julai 14 na 18 dhidi ya Simba.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Morocco alisema mechi zilizipo mbele yao ni ngumu na wanahitaji kupata pointi sita kwa lengo la kumaliza ligi wakiwa kwenye nafasi ya nne.

"Kwa sasa tuna pointi 43, kufikia nafasi ya nne za juu lazima nishinde mechi zote hizo, tunahitaji kupambana na hali ambayo akili na nguvu kuelekeza katika malengo hayo bila kujali aliyekuwa juu yetu anafanya nini," alisema.

"Kwanza tunahitaji kushinda mechi zetu, tunacheza na Ruvu Shooting ni wazuri pia tunakuja kumaliza ligi dhidi ya Simba, zote ni mechi ngumu na ushindani mkubwa tunatakiwa kushinda ili kufikia malengo yetu hayo ya msimu ujao kucheza kombe la Shirikisho," alisema Morocco.

Alisema kufikia malengo hayo lazima wapambane na kushinda mechi hizo na kupambania nafasi ya nne ambayo itawaweka mazingira ya kucheza kimatifa.

# TUKO TAYARI KWA FAINALI - MWAMMNYETO

**Na Adam Fungamwangwo**

BAADA ya kutinga hatua ya fainali kwa kuichapa Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi mjini Tabora, nahodha wa Yanga, Bakari Mamnyeto amesema yeye na wachezaji wenzake wako tayari kwa fainali.

**Akizungumza mara baada ya mechi hiyo kumalizika, beki huyo wa kati alisema kwenye mechi hiyo hali ya hewa ilichangia sana wao kupata ushindi kiduchu.**

"Hali ya hewa ilichangia sana kipindi cha pili sisi kukata upepo, ndiyo maana unaona wapinzani wetu walitushambulia sana, lakini tunashukuru kwa kupata pointi tatu," alisema.



Kuhusu mechi ya fainali, alisema wao tayari wameshatinga hatua hiyo, hivyo wako tayari kwa mechi hiyo inayotarajia kupigwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, mjini Kigoma.

"Sisi tuko tayari kwa fainali, wala hatuna matatizo lolote." Alisema.

Naye nahodha wa Biashara United, Abdulmajid Mangalo alisema walijitahidi kwa kadri ya uwezo wao, lakini wameshindwa.

"Tumefungwa kimchezo tu, unajua tulianza taratibu sana, jamaa wakatuwahi. Tulijitahidi kipindi cha pili kufunguka baada ya kocha wetu kutuambia kuwa wakitushambulia na sisi tushambulie. Kweli tuliwakamata kipindi cha pili, lakini hatuweza kutumia nafasi ambazo tulizipata kama ile kipa aliyocheza na moja ikagonga mwamba," alisema Mangalo ambaye anahusishwa kujiunga na klabu tatu kubwa nchini, Simba, Yanga au Azam FC mwishoni mwa msimu.




Bondia Ranjit Maige (kushoto) na Oscar Kitale, wakitwishana ngumi wakati wa bonanza la uzinduzi wa Gym Kivule jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Wafia dansi yaipaisha Waluguru*

**Na Sabato Kasika**

BENDI ya muziki wa dansi ya Waluguru Original ya mjini Morogoro, imesema, onyesho maalum la 'Wafia dansi' lililofanyika hivi karibuni mjini humo, limeiongezea umaarufu na kujipatia mashabiki wengi zaidi.

Mkurugenzi wa bendi hiyo, Killer Man aliliambia gazeti hili kuwa, tangu kufanyika kwa onyesho hilo, Waluguru Original imekuwa aikipata mialiko mingi ya kutoa burudani mjini humo.

"Tulitumia vizuri onyesho hilo lililokuwa na lengo la 'kufufua' muziki wa dansi, kwa kuburudisha mashabiki wa dansi inavyotakiwa na sasa wanaendelea kujitokeza kwa wingi katika maonyesho yetu," alisema.

Alisema, pamoja na kwamba onyesho hilo lilishirikisha bendi tatu ikiwamo ya Bogos kutoka jijini Dar es Salaam, Sky Melody ya jijini Dodoma na vikundi vingine, anaamini limesaidia kuwaongezea mashabiki.

"Kwa ujumla, tulitumia fursa hiyo vizuri ya kuwafanya mashabiki wa muziki wa dansi kujua kuwa Waluguru Original tuko vizuri na pia muziki huu bado una nguvu ingawa haupewi nafasi kubwa kama zamani," alisema Killer Man.

Alisema, kwa sasa wanajipanga kutanua maonyesho yao hadi kwenye miji mbalimbali ikiwamo pia jiji la Dar es Salaam, na kwamba ikiwezekana wataandaa bonanza la kila Jumapili katika jiji hilo.

Mkurugenzi huyo alisema, kwa sasa bendi yake inataamba na albamu mpya iitwayo 'Kikao cha Wahenga' yenye nyimbo za 'Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe'.

Alisema, wimbo wa 'Morogoro Yetu', unaelezea sifa za mkoa wa Morogoro wenye milima ya kupendeza, na kwamba albamu yao ni maalum kwa ajili ya kuhamasisha muziki wa dansi ili urejee kwenye chati.

# Michezo

Jumapili Juni 27, 2021

Nipashe




Sancho akaribia kusaini Man Utd UKURASA 22



Iddy Seleman 'Nado' wa Azam FC (kushoto), akiwania mpira na Shomari Kapombe wa Simba wakati wa mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA, uliopigwa jana uwanja wa Majimaji mjini Songea. Simba ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

## Nabi: Malengo ya Yanga kubeba kombe

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema kazi iliyopo mbele yake ni kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake kwa ajili ya kucheza fainali na kutwaa ubingwa wa Kombe la Shikisho.

Yanga juzi ilitinga fainali baada ya kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Biashara United, bao pekee limefungwa na Yacouba Songne.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anafanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mchezo iliyopita na kujiimarisha zaidi kwenye mchezo wao wa fainali na kuhakikisha wanatwaa taji hilo.

Alisema tayari wana uhakika wa kucheza fainali na hali ambayo malengo yao makubwa kufikia hatua hiyo sasa wanafanyia kazi mapungufu yao na kutaka kutwaa taji hilo ambalo linashikiriwa na Simba.

"Siwezi kuzungumza mpinzani wangu, tunafurahi kufikia fainali, wachezaji wamepambana na sasa tunarejea mazoezini kufanyia kazi mapungufu yetu," alisema Nabi.

Licha ya kujivunia timu yake kucheza vizuri na kuona mabadiliko makubwa, pia amempa majukumu mengine kiungo wake, Feisal Salum 'Fei Toto' kucheza nafasi ya kiungo mchezeshaji. Nyota huyo ameeanza kuzoea majukumu yake mapya na sasa yanga imeanza kuonyesha sura tofauti inaposhambulia.

Nabi amemtumia Fei Toto kucheza kiungo mchezeshaji katika miechi tatu akianza kwenye dhidi ya Ruvu Shooting na akafunga mabao mawili.

Pia alicheza katika nafasi hiyo kwenye mchezo dhidi ya Mwadui akasaidia kupata ushindi wa mabao 3-2 na amemtumia katika mechi ya nusu fainali ya Shirikisho dhidi ya Biashara United na amechangia Yanga kuondoka na ushindi wa bao 1-0.

Pasi ya Fei Toto katika dakik 22 ya kipindi cha kwanza ilitumiwa na Yocouba kufunga bao pekee ambalo limewapeleke fainali.

# Simba yaifuata Yanga FA

## ●●● Yatinga fainali baada ya mechi kali iliyojaa ufundi, nguvu, ubabe...

**Na Adam Fungamwango**

RASMI sasa Simba na Yanga zinakwenda kucheza fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) maarufu kama Kombe la FA kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma.

**Hii na Baada ya Simba jana jioni kwenye Uwanja wa Majimaji, Songea mkoani Ruvuma kutinga fainali hiyo, ilipoichana Azam FC bao 1-0 kwenye mechi kali, iliyojaa ufundi, nguvu na ubabe pia.**

Ilionekana kama inaweza kuchezwa kwa dakika 120, lakini dakika mbili kabla mechi hiyo kukamilika kwa dakika 90, Simba ilipata bao pekee kwenye mechi hiyo.

Luis Miquissone alipata pasi fupi ya faulo kutoka kwa Bernard Morrison na kuupiga mpira kiufundi, ukawapita kipa Mathias Kigonya wa Azam na mabeki wake, ukajaa wavuni.

Faulo hiyo ilitokana na Morrison kufanyiwa faulo na Bruce Kangwa nje kidogo ya eneo pembeni mwa eneo la hatari.

Bao hilo liliamsha hoi hoi na nderemo kutoka kwa mashabiki wa Simba waliojazana kwa wingi kwenye uwanja huo.

Hata hivyo, wachezaji wa Azam walimzonga mwamuzi, Ahmed Arajiga kutoka Manyara kwa madai Morrison alianzisha mpira kabla hawajajipanga.

Marudio ya picha za televisheni yalionyesha kuwa mwamuzi huyo aliamuru faulo ipigwe. Kosa la wachezaji wa Azam walionekana kwenda kwa mwamuzi kabla ya faulo kupigwa kuliko kuzuia na kuwakaba wachezaji wa Simba.

Kwenye mechi hiyo, Simba ilianza kuliandama lango la Azam kuanzia mwanzo wa mchezo, hadi dakika ya 30, Azam ilipozinduka.

Mzamiru Yassin aliikosesha Simba bao dakika ya tatu tu ya mchezo, baada ya kupata pasi safi kutoka kwa Clatous Chama na akiwa nje kidogo ya eneo la mita 18 aliachia shuti kali lililotoka pembeni kidogo la lango la Azam.

Dakika ya 16, Thadeo Lwanga alikosa bao la wazi baada ya kupiga kichwa akiwa hajakabwa na walinzi wa Azam, lakini mpira ulitoka nje. Shambulio hili lilitokana na mpira wa adhabu uliopigwa na Shomari Kapombe, kufuatia Daniel Amoah kumchezea vibaya Luis Miquissone.

Azam ilifanya shambulio la kwanza kali kwenye lango ya Simba dakika ya 30, baada ya shuti kali ya Salum Aboubakar kupanguliwa kwa ustadi na kipa Aishi Manula aliyekuwa likizo kwa muda mrefu.

Sure Boy, alimegewa mpira wa kona iliyopigwa na Idd Nado akiwa nje kidogo ya eneo la hatari.

Kipindi cha pili, pamoja na kufanya mabadiliko ya wachezaji, timu zote zilionekana kucheza mchezo uliofanana kwa kupiga mipira mirefu na kushambuliana kwa zamu, hadi ilipofika dakika ya 88.

Simba itacheza na Yanga ambayo siku ya Ijumaa ilifanikiwa kuingia hatua hiyo kwa kuidungua Biashara United bao 1-0 kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mjini Tabora.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >